**TANESCO** yadai Bil. 224/- madeni umeme, Biteko aagiza wakatiwe

UKURASA 2

**TAMWA** yakumbusha wazazi umakini katika malezi ya watoto

UKURASA 5



**RC** Mtaka atishia kucharaza viboko wazazi na walezi

UKURASA 16

UKURASA 22



**KLOPP AFURAHIA SARE NA MAN CITY**


# Nipashe

Jumatatu Novemba 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581507

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


KASHFA UDHALILISHAJI

# Mbunge akamatwa



• **Ni** baada ya Samia kutengua uteuzi uwaziri, Lema, asasi wataka avuliwe ubunge, uanachama CCM... *Ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### SERIKALI YAIPONGEZA KAMPUNI YA BIMA KWA KUKINGA MAJANGA



KAMISHNA wa Bima nchini, Dk. Baghayo Saqware, ameipongeza kampuni ya bima ya Britam kwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya bima nchini...



Mtoto akitekeleza majukumu ya kijamii wilayani Bunda, mkoani Mara Jumatatu Novemba 13, mwaka huu saa 5:42 asubuhi, muda ambao alipaswa kuwa darasani. **PICHA: SANULA ATHANAS**

## Ajali ya basi ilivyokatisha uhai watu 14, kujeruhi 26

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM

## Halmashauri Wilaya ya Bunda na maisha hasi kwa watoto

UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA YAIONYA AL AHLY KWA MKAPA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (kushoto), akipokea tuzo baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa Tuzo za Umahiri Nyanja za Uongozi kundi la Hifadhi ya Jamii, katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KASHFA UDHALILISHAJI

# Mbunge akamatwa, ahojiwa

**Na Waandishi Wetu**

MBUNGE wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, amekamatwa na kuhojiwa na Jeshi la Polisi saa chache baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutengua uteuzi wake katika nafasi ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP), George Katabazi, alipotafutwa na Nipashe jana jioni kuzungumzia suala hilo, majibu yake yalikuwa hivi:

**Mwandishi:** Kamanda (Katabazi), taarifa za Pauline Gekul kukamatwa akidaiwa kujaribu kutoroka kwenye Mpaka wa Namanga ni za kweli?

**Katabazi:** Si za kweli, ni watu tu wameandika kwenye mitandao, hata mimi nimeona kuna mtu ametengeneza tu.

**Mwandishi:** Kuna taarifa pia kwamba kuna wananchi wenye hasira walionekana asubuhi kuvamia makazi ya Gekul. Zina ukweli?

**Katabazi:** Si za kweli, wangepiga picha tuone hao wananchi waliovamia makazi ya mtuhumiwa?

**Mwandishi:** Ni hatua gani mnazoendelea nazo juu ya Gekul kumfanyia ukatili Hashim Ally?

**Katabazi:** Tunaendelea na uchunguzi.

**Mwandishi:** Yeye Gekul ameshahojiwa?

**Katabazi:** Toka asubuhi, nimeacha wanamhoji Ofisi ya RCO (Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkoa wa Manyara).

**Mwandishi:** Unawaambia nini wananchi ambao wana taharuki juu ya tukio hili?

**RPC:** Wawe watulivu, waliamini Jeshi la Polisi, litafanya kazi yake ya uchunguzi kwa weledi. Tulikuwa tunamhoji, polisi hatuwezi kumhoji nyumbani kwake.

**Mwandishi:** Askari waliohusika wamechukuliwa hatua gani?

**Katabazi:** Tunaendelea na uchunguzi juu yao, tukikamilisha tutachukua hatua.

**Mwandishi:** Baada ya kuhojiwa, mmeendelea naye Gekul au amerudi nyumbani kwake?

**Katabazi:** Niliacha wanamhoji, walikuwa wanaendelea naye.

**LEMA APONGEZA**

Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini (CHADEMA), Godbless Lema, amempongeza Rais Samia kwa hatua za haraka alizochukua dhidi ya kiongozi huyo kwa kutengua uteuzi wake katika nafasi ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

Alisema hatua hiyo ilichukuliwa na Rais Samia baada ya kuenea taarifa katika mitandao ya kijamii, akidaiwa kuhusishwa na kitendo cha ukatili dhidi ya kijana mmoja mkoani Manyara, anayedaiwa kuingizwa chupa ya soda sehemu ya siri.

Lema alisema jana kuwa anampongeza Rais Samia kwa sababu ameona na amesikia kilio cha wananchi wanyonge dhidi ya ukatili huo.

"Huu ni ukomavu wa akili na uungwana alioufanya Rais kwa kuchukua hatua za haraka hivi za kumtengua unaibu waziri. Ninampongeza amefanya jambo jema na la kiuungwana.

"Kweli nimejisikia vibaya sana juu ya taarifa hii kwani ningekuwa mimi kijana wangu amefanyiwa hivi na kiongozi kama huyu, ninadhani leo ningepata kesi kubwa maana ningeshindwa kujizuia," alisema Lema akimwombea Rais Samia baraka kwa Mungu.

Hata hivyo, Lema alisema kuna haja hatua zingine zichukuliwe, ashtakiwe kwa kuwa hiyo ni kesi ya jinai.

"Ninatoa rai kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumchukulia hatua ya kumvua uanachama na kumvua ubunge kwa sababu huyu si raia mwema, hastahili kuendelea kuwa katika chama kama hiki kinachoshika dola," alidai.

Lema pia aliomba uongozi wa Jeshi la Polisi ngazi ya kitaifa, nao uchukue hatua dhidi ya uongozi wa polisi mkoani humo kwa kutaka kuficha kitendo hicho.

Alisema CCM ikimfukuza na kumvua nyadhifa zake kitatoa matumaini kwa umma.

Wakati hayo yakiendelea kaskazini mwa nchi, mkoani Iringa jana mashirika yasiyo kuwa ya kiserikali yalitaka CCM kuchukua hatua za kumvua ubunge na uanachama Gekul.

Katibu wa shirika lisilo la kiserikali la ICISO, Raphael Mtitu na Katibu Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Caringi Hearts (CAHE), Jameda Kulanga walisema hatua iliyochukuliwa na Rais Samia imezingatia utawala bora.

Walisema ni muhimu chama chake kinachomdhamini ubunge, kichukue hatua za haraka kama ambavyo Rais alivyochukua hatua haraka ili kutoa fundisho kwa wabunge na viongozi wengine.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, alitoa taarifa yenye aya moja juzi usiku, akitangaza kutenguliwa kwa uteuzi huo. Hata hivyo, taarifa hiyo ya Ikulu haikutaja sababu za uamuzi huo wa Rais Samia.

Katibu wa Mbunge huyo, Hussein Abrima, alikaririwa na vyombo vya habari jana akikanusha tuhuma dhidi ya Gekul, akitaja madai ya udhalilishaji yana mrengo wa ushindani wa kibiashara. Alisisitiza suala hilo linashughulikiwa na Jeshi la Polisi.

Gekul ambaye ni Mbunge wa Babati Mjini, kwa mara ya kwanza aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Desemba 5, 2020; chini ya uongozi wa Hayati Dk. John Magufuli.

Mnamo Machi 2021, Rais Samia alipofanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri, alimteua Gekul kuwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Alitumikia nafasi hiyo hadi Februari 23, mwaka huu alipoteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

Kabla ya kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Gekul alikuwa mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambako pia alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA) Mkoa wa Manyara, pia alikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa Kanda ya Kaskazini waliotokana na chama hicho.

Mnamo Oktoba 2018, Gekul alijivua uanachama wa CHADEMA na kujiuzulu nafasi zake zote za uongozi kisha kujiunga na CCM. Alitaja sababu za kufanya hivyo ni kile alichodai CHADEMA kuwabebesha wabunge mzigo wa ujenzi wa chama.

***Imeandikwa na Jaliwason Jasson (MANYARA), Godfrey Mushi, Cynthia Mwilolezi (ARUSHA) na Francis Godwin (IRINGA).**

# TANESCO yadai bil. 224/- madeni umeme, Biteko aagiza wakatiwe

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kukata umeme kwa wadaiwa jumla ya Sh. bilioni 224 kutoka taasisi mbalimbali za serikali, binafsi na waliohama na madeni.

Alisema hayo jana wilayani Arumeru, mkoani Arusha, alipokagua kituo cha umeme cha Lemuguru ambacho ujenzi wake ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa njia kuu ya msongo wa kV 400 kutoka Singida mpaka Namanga kuelekea Kenya (Kenya-Tanzania Power Interconnection Project (KTPIP).

"Hapa Arusha tu, TANESCO anadai wateja wake Sh. bilioni 7.7 na mara nyingi wanaodaiwa si wananchi wadogo ni taasisi za serikali na wawekezaji wanaojiita wakubwa ambao ukiwakatia wanakwambia unaua ajira, wepesi wa kujificha kwenye kisingizio cha kulipa kodi na ajira," alisema.

Dk. Biteko alisema TANESCO inahitaji fedha ili iwekeze na kuwapelekea umeme wananchi na kuagiza kumkatia mtu yeyote anayedaiwa.

Pia ameagiza wadaiwa wote wa madeni ya bili za umeme wakalipe madeni hayo ili zipatikane fedha za kuwahudumia wananchi na serikali itaendelea kushughulikia changamoto za umeme nchini kwa aina mbalimbali ikiwamo kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji wa nishati hiyo ukiwamo wa Julius Nyerere (MW 2115), ambao umefikia asilimia 94 na mkandarasi ameshafunga mashine mbili kuanza majaribio ya kuzalisha umeme.

Katika hatua nyingine, Dk. Biteko alikemea watu wanaohujumu miundombinu ya umeme akitoa mfano wa wizi wa nyaya za shaba na mafuta.

Alisema kati ya Novemba 25 na 26, 2023 kuna matukio 14 katika Ukanda wa Pwani ya kuharibu au kuhujumu miundombinu ya umeme, na kuonya serikali itawashughulikia kwa kuendesha msako na watakaopatikana sheria itachukua mkondo wake.

Aidha, Dk. Biteko ameitaka TANESCO kuwasikiliza na kuwapatia majibu haraka wananchi wanaopiga simu ili kupata huduma za umeme na mahali penye matatizo waambiwe, "huu utaratibu wa watu kupiga simu anaambiwa subiri, hii tumekubaliana kuwa haiwezekani ikaendelea na ndio maana nimewaambia kituo cha 'Huduma kwa Mteja' tukiimarishe kutoka miito 65 na ziongezwe kufika 100 na zaidi."

Kuhusu utekelezaji wa kituo hicho cha umeme cha Lemuguru, Dk. Biteko alisema mradi huo ni mkubwa na unagharimu Dola za Marekani milioni 258.8 na kina faida mbalimbali ikiwamo kupelekea wananchi umeme usiokatika mara kwa mara na kituo kitaimarisha hali ya umeme mkoani Kilimanjaro na Arusha.

Aliipongeza TANESCO kwa hatua mbalimbali inazochukua ili kupunguza makali ya mgawo pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kuongeza kiwango cha Gesi Asilia kinachozalisha umeme.

Awali, akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wenye msongo wa Kilovoti 400 kutoka Singida hadi Namanga kuelekea Kenya, Msimamizi wa Mradi huo, Mhandisi Peter Kigadye, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kuongeza uwezo wa kusafirisha umeme kwenda mikoani na migodi ya uchimbaji madini na kuwezesha kufikia uwezo wa juu wa megawati 2000 kusafirisha nishati hiyo.

Alisema, utekelezaji wa mradi unahusisha vipengele sita ikiwamo ujenzi wa njia nane za laini ya kV 400/33 kutoka kituo kipya cha kupoza umeme, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha yenye urefu wa kilomita 414.3, Babati -Arusha kilomita 150, Arusha -Namanga, Kilomita 114.3 ambao umefikia asilimia 96.

Mradi huo pia unahusisha, upanuzi wa vituo vya kupoza umeme ambao umefikia asilimia 98.72, mradi wa usambazaji umeme kwa vijiji vilivyopitiwa na mradi vijijini na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Dodoma, Singida, ambavyo vimekamilika.

HABARI KITAIFA



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali Venance Mabeyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM ataka ushirikiano kukabili ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka jamii kushirikiana na serikali na asasi za kiraia kupambana na matendo ya ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wenye ulemavu.

Amesema ili kupata matokeo ya haraka, wanajamii wahusishwe kuanzia hatua ya upangaji wa mikakati ambayo itatumika kutekeleza afua zinazohusu jamii yao.

"Namna hii itawawezesha kuzikubali afua hizo na kujiona kuwa ni sehemu muhimu katika utekelezaji. Wanajamii wasipangiwe bali washirikishwe kupanga mikakati inayohusu jamii zao."

Aliyasema hayo jana wakati alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika mbio za hisani za kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, watoto na wenye ulemavu (Stop gender based violence) zilizohitimishwa katika viwanja vya Forodhani, mjini Zanzibar.

Aidha, Waziri Mkuu aliziagiza idara na mashirika ya serikali kuimarisha ushirikiano na asasi za kiraia zinazotekeleza afua za kutokomeza ukatili wa kijinsia.

"Kwa kuwa serikali zimeshaandaa mipango na mikakati ya kitaifa, asasi za kiraia zitekeleze shughuli zao kwa kuzingatia mipango hiyo ili kuharakisha utatuzi wa changamoto za kijinsia."

Alisema serikali katika kutekeleza Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya mwaka 2017, imewezesha makundi maalum yakiwamo ya wanawake na watoto kupata haki zao katika vyombo vya usimamizi wa sheria.

"Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikitoa msaada wa kisheria kwa waathirika wa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia ambapo zaidi ya waathirika 1,700 wamepatiwa msaada wa kisheria na kisaikolojia katika mwaka 2022/2023."

Kadhalika, serikali imeunda madawati na vituo kwa ajili ya ulinzi na usalama wa mtoto na kutoa huduma za msingi kwa waathirika wa matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Kwa upande wa Tanzania Bara; madawati 1,850 katika shule za msingi 1,128 na sekondari hadi kufikia Septemba 2023. Kwa upande wa elimu ya kati na elimu ya juu madawati 273 yameanzishwa hadi kufikia Juni 2023."

Alisema kwa upande wa Zanzibar jumla ya madawati 40 yameundwa katika vituo vya polisi ili kuharakisha utoaji huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia. Aidha vituo saba vya kutolea huduma za mahali pamoja vimeanzishwa Mnazi Mmoja, Makunduchi na Kivunge; Pia Wete, Mkoani, Chakechake na Micheweni.

Pia aliziagiza Idara na Mashirika ya Serikali yaimarishe ushirikiano na asasi za kiraia zinazotekeleza afua za kutokomeza ukatili wa kijinsia.

"Kwa kuwa serikali zimeshaandaa mipango na mikakati ya kitaifa, asasi za kiraia zitekeleze shughuli zao kwa kuzingatia mipango hiyo ili kuharakisha utatuzi wa changamoto za kijinsia."

Waziri wa Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, alisema Serikali ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, imejizatiti kuhakikisha inadhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Asma Foundation, Asma Ali Mwinyi, alisema mbio hizo za hisani zimelenga kukusanya Sh. milioni 500 ambazo zitatumika kuwawezesha wanawake, watoto na wenye ulemavu waliopata changamoto za unyanyasaji wa kijinsia.

# Ajali ya basi ilivyokatisha uhai watu 14, kujeruhi 26

**Na Waandishi Wetu**

WATU 14 wamefariki dunia huku wengine 26 wakijeruhiwa kutokana na ajali ya basi la Kampuni ya Baraka iliyotokea jana saa moja asubuhi katika Kitongoji cha Mputa, Kijiji cha Mtama, mkoani Lindi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Kamishna Msaidizi John Imori, kati ya watu 14 waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo, 12 ni abiria wa basi hilo na wawili ni watembea kwa miguu waliogongwa na basi hilo wakati wa ajali.

Alibainisha kuwa chanzo cha ajali hiyo ni breki za basi hilo kufeli wakati likiteremka katika Mlima wa Kirorambendo. Lilikuwa linatoka Newala mkoani Mtwara kwenda Dar es Salaam.

Kamanda Imori alisema miili ya waliofariki dunia imehifadhiwa katika Hospitali ya Nyangao huko Mtama. Majeruhi wa ajali hiyo pia walikuwa wanapatiwa matibabu katika hospitali hiyo.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo na wenyeji wa Mtama, walisema eneo ilikotokea ajali hiyo hilo lina kona kali na mteremko ambao ni hatari kwa watumiaji wa barabara hiyo. Waliomba serikali ipunguze ukali wa kona hiyo.

Daktari katika Hospitali ya Nyangao, Dk. Julius Stephen, alimwambia mwandishi kuwa walipokea majeruhi 26 jana saa mbili asubuhi. Kati yao, baadhi waliitibiwa na kuruhusiwa kutoka hospitalini, lakini saba wamelazwa kwa ajili ya matibabu zaidi.

Dk. Stephen pia alibainisha kuwa walipokea miili ya watu 14 waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo.

Alisema kuwa miili bado haijatambuliwa na kwamba mmoja wa majeruhi saba, hali yake ilikuwa mbaya na alikuwa amelazwa Chumba cha Wagonjwa Wanaohitaji Uangalizi Maalum (ICU).

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, mwaka jana (2022) vifo vya watu 1,720 vilitokea kutokana na ajali za barabarani nchini.

**Imeandaliwa na Said Hamdani na Julieth Mkireri**


**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



BWANA **LACKISON LUDOVICK KAHWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA "PASSPORT YENYE NAMBA **TAE364764** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILI CHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/DAR/ILA/43825/2023.**



**The United Republic of Tanzania**
**President's Office**

09.11.2023

**VACANCY ADVERTISEMENT**

**EXTENSION OF DEADLINE FOR SUBMISSION**

Tanzania Social Action Fund (TASAF) is currently implementing Productive Social Safety Net Program which aims at protecting the Vulnerable Poor Households from severest consequences of poverty by implementing interventions that will lead to increased Household incomes and opportunities while increasing consumption.

The Permanent Secretary, President's Office, State House advertised a vacant post for TASAF Executive Director from 10th October 2023 and the deadline was 10th November 2023.

The general public is hereby informed that the deadline for submission has been extended from 10th November 2023 to 27th November 2023.

All other details remain as they were advertised in the original invitation.

PERMANENT SECRETARY
PRESIDENT'S OFFICE, STATE HOUSE

RIPOTI MAALUM

# Wilaya ya Bunda na maisha hasi kwa watoto

**Na Sanula Athanas aliyekuwa BUNDA**





Baadhi ya watoto katika eneo la Kasuguti wilayani Bunda mkoani Mara wakiendelea na shughuli za kijamii Jumatatu Novemba 13, mwaka huu asuhuhi, muda ambao walipaswa kuwa shuleni. **PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**

ANGALIA ulimwengu wa watoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda mkoani Mara: Mmoja anachunga ng'ombe; mwingine anakwenda ziwani kuvua na kuuza samaki; mwingine yuko shambani analima; mwingine amekosa mahitaji ya shule, anarandaranda mitaani; mwingine ameolewa; mwingine anafanya kazi katika baa; mwingine bibi yake amesema akisomeshwa watamroga; na mwingine yuko mgodini anachimba madini.

Kati ya mwaka 2018 na 2021, waliandikishwa watoto 13,625 kujiunga na elimu ya msingi; lakini 7,565 (asilimia 55) waliacha shule.

Mwaka jana, wanafunzi 1,717 walikatisha masomo. Hii ni sawa na asilimia 15 ya wanafunzi 11,233 waliopaswa kuwa shuleni. Mwaka huu (2023), wanafunzi 994 wamejiunga mtaani. Hao ni sawa na asilimia 9.6 ya wanafunzi 10,343 waliopaswa kuwa shuleni katika halmashauri hiyo.

**SHIDA NI NINI?**

Ofisa Elimu Taaluma Idara ya Elimu Msingi na Awali katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Didas Mgaya, anasema mfumo wa uchumi wa wakazi; unaotegemea watoto katika uzalishaji shambani, uvuvi, ufugaji na uchimbaji madini, unachangia watoto kuacha shule.

Mgaya anataja pia kile anachoita "fikra duni" ambazo wazazi wanazipa kipaumbele kuliko masomo na kwamba zinachangia watoto wao kuacha shule. Anataja shughuli za uvuvi, ufugaji na kilimo zinapewa kipaumbele kuliko shule.

"Hali ya mdondoko wa wanafunzi katika halmashauri yetu ni kubwa kutokana na shughuli mbalimbali za kijamii. Mwaka 2022, walioacha shule ni 1,717 kati ya wanafunzi 11,233 walioandikishwa. Kwa mwaka huu (2023), walioacha ni wanafunzi 994 kati ya 10,343.

Wanaokumbwa na mdondoko ni wavulana kwa sababu ndio wanaohusishwa sana katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Shule zilizoko kando ya ziwa (Victoria), hasa ukanda wa chini wa uvuvi, ndizo zenye idadi kubwa ya wanaoacha shule.

"Zote ni za Jimbo la Mwibara, ambako shule ya Mwinguma ina idadi kubwa ya wanafunzi wanaoacha shule. Ukanda wa juu, kuna Shule ya Msingi Nyaburundu. Huko ndiko shughuli kubwa ni ufugaji na kilimo; nayo ina idadi kubwa ya wanaoacha shule. Eneo hilo pia lina migodi midogo ya dhahabu. Wavulana wanatokomea huko," anafafanua.

Ili kukabiliana na tatizo hilo, Mgaya anasema wameelekeza Maofisa Elimu Kata, kwa kushirikiana na walimu wakuu, kuandaa orodha ya wanafunzi wanaoacha shule na kuikabidhi kwa Maofisa Watendaji wa Kata na Vijiji ili kuchukua hatua za kisheria.

Mgaya anasema pia kwamba wanashirikiana na shirika lisilokuwa la kiserikali la Project Zawadi, ambalo sasa limejikita Bunda kusaidia upatikanaji mahitaji kwa watoto wanaotoka familia duni kiuchumi.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Maria John, anasema kushamiri kwa ndoa za utotoni, zinazoingia katika kipaumbele cha mila za wakazi wa eneo hilo, kunachangia watoto kukatisha masomo katika eneo lake la kazi.

Maria pia anautaja mfumo wa malezi kuwa ni tatizo. Watoto wengi wanalelewa na bibi zao ambao uelewa wao kuhusu shule na elimu, uko chini. Anataja tatizo lingine kuwa ni wazazi wanaohamahama, kutokana na shughuli zao za ufugaji na uvuvi. Wanahama ili kutafuta malisho mapya, hata samaki.

Anasema "Mzazi anapohama, hahami na familia nzima; anaacha watoto kwa bibi au ndugu wengine kisha kuwatelekeza huko. Kuna mtoto anaacha shule kisa tu shati limechanika. Watoto wa aina hii wapo.

Tunapobaini, tunawakumbusha walezi na wazazi wajibu wao kutekeleza haki ya mtoto. Kama mtoto ametelekezwa, tunamuunganisha na ndugu ili ahudumiwe."

Maria anafafanua kuwa kama ndugu nao hawana uwezo, "inabidi tumpeleke mtoto kwenye makazi ya kulea watoto. Huko tuna watoto wengi wakiwamo ambao wazazi wameshafariki dunia. Tunao watoto 135 kwa sasa katika makazi yetu," anasema.

Ofisa Ustawi wa Jamii huyo anaeleza athari za watoto kuacha shule kuwa zinajumuisha kukosa haki ya kupata elimu, uwezo wa kujiajiri na kujitambua.

"Mtoto anayekosa fursa ya kupata elimu, anakuwa mtu ambaye hajapata chochote. Ndoa za utotoni zinawaandama. Anapokosa elimu anakuwa nyumbani, eneo letu hili, hasa ukanda wa juu ndoa za utotoni ni nyingi.

"Mtoto anakuwa na uwezo mdogo wa kujisimamia, mwisho wa siku hutelekeza watoto kwa sababu wanashindwa kuwalea. Kesi za watoto waliotelekezwa zipo kwa kiwango kikubwa. Kuna wengine wanazaa ilhali hawakuwa na malengo ya kuwa pamoja," anafafanua Maria.

Maria anabainisha mikakati ya kudhibiti mdondoko shuleni kuwa inajumuisha kutoa elimu ngazi ya jamii juu ya kulinda watoto. Elimu hiyo wanaitoa kupitia midahalo shuleni, madawati na mabaraza waliyoanzisha kwa lengo la kuwasikiliza watoto na kutambua shida zao.

"Tumeweka utaratibu kila shule iwe na mwalimu anayetoa nasaha kwa watoto. Kuna chumba maalum kwa ajili ya nasaha katika shule zote za Bunda DC," anasema.

Walimu wa kike na wa kiume wilayani Bunda hawako mbali na kilichoelezwa na viongozi wao. Mbali na mengi yaliyoorodheshwa, wanataja umaskini unaondoa mazingira rafiki ya masomo; na watoto kukosa mahitaji ya msingi yanayowawezesha kusoma.

Mwalimu wa Michezo na Nidhamu katika Shule ya Msingi Mwibara,

Flora Kalalo, anakosoa mila na tabia binafsi za wazazi wanaotelekeza watoto, akielekeza kidole chake kwa wazazi wa jinsia yake waliojikita katika starehe ndani ya visiwa vya Ziwa Victoria.

"Kuna kinamama wanazaa na kuacha watoto huku vijijini. Wanazunguka tu kwenye starehe za visiwani. Hawa nao ni vyanzo vya watoto kukosa malezi na kushindwa kuendelea na masomo," anasema Mwalimu Flora.

Mwalimu Mkuu Msaidizi katika Shule ya Msingi Mwibara, Charles Onyango, anaunga mkono hoja hiyo ya mwalimu mwenzake, akisisitiza starehe hizo zina mchango mkubwa katika kudidimiza elimu.

"Mazingira ya nyumbani kwa watoto wengi si rafiki na yanachangia kuacha shule; kwa sababu akifika shuleni, anawaza matatizo yaliyoko nyumbani.

Na shughuli kubwa kwa wakazi wa hapa ni uvuvi.

Unakuta mtoto yupo shuleni lakini anawaza akirudi nyumbani, aende ziwani kuvua samaki.

"Watoto wengi hawakai na wazazi wao. Wanakaa na welezi kama vile bibi, shangazi, mama mdogo au mtu wa karibu. Sasa, mlezi anashindwa kuwahimiza kwenda shuleni, mwisho wa siku mtoto anaathirika, anaangalia afanye shughuli gani ili kuwa na kipato," anafafanua.

ZIli kunusuru watoto kukosa haki ya kupata elimu, Mwalimu Onyango anashauri serikali na wadau wa elimu na ustawi wa jamii waandae semina anazozita "elekezi," hususan katika mazingira ya wavuvi na wafugaji, ili watambue umuhimu wa watoto wao kupata elimu.

Sasa safari ya mwandishi inahamia kwa wanaonyooshewa kidole na kutwishwa lawama. Ni kwa mzazi wa watoto wanane na mume wa wake wawili, Mussa Masanja (34), ambaye anakiri mdondoko umekithiri kwa wanafunzi wa shule za msingi za Kata ya Kasuguti ambako anaishi.

Masanja, mzaliwa wa Bariadi mkoani Simiyu, anatumia mfano binafsi. Kimasomo aliishia darasa la kwanza. Sababu kuu ni kuweka kipaumbele kwenye ufugaji. Mlezi wake ambaye ni kaka yake, alimtelekeza katika umri mdogo, akimwachia baadhi ya mifugo aendelee nayo; yeye akihamia kusini mwa nchi, Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi.

"Sisi wazazi tunategemea watoto kutusaidia baadhi ya shughuli za nyumbani. Ninatamani wanangu wote wasome, lakini wakati mwingine inabidi wasiende shuleni, wananisaidia kuchunga ng'ombe.

"Mimi niliishia darasa la kwanza.

Nilikataa mwenyewe kuendelea na shule kwa sababu niliona sina kipaji cha kusoma. Hata hapa kijijini wapo watoto wengi tu wanaokataa kusoma. Wamejikita kwenye uvuvi, wengine wanalima na wengine tunafanya nao shughuli za ufugaji," anasema Masanja.

Naye mzazi wa kike, Leticia Matekele, anasimama kwenye hoja ambayo Ofisa Ustawi wa Jamii Flora amesita kuitolea ufafanuzi, kwamba kusoma zaidi kuna hatari ya mwanafunzi kupigwa vita ikiwamo kurogwa.

Hii ni imani ambayo mkazi huyo wa Kata ya Kasuguti anasema ina nguvu katika mila za jamii yao, hivyo mbadala salama ni mtoto kubaki nyumbani.

"Watu wa huku wanaamini ukisomesha sana mtoto atarogwa. Sasa uamuzi unabaki juu ya mzazi; 'nimsomeshe mwanangu wamroge au aache shule ili aendelee kuwa hai," anatamka Leticia ambaye ni mama wa watoto watatu (wawili wa kike). Mmoja wa wanawe anasoma darasa la awali, lakini mahudhurio yake ni ya kusuasua. Wawili hawajafikia umri wa kuwa shuleni.

Katika tathmini ngazi ya familia, mwandishi alipata majibu toka kwa mtoto mwenye umri wa miaka 10 (jina tunalo) aliyekutwa porini kwenye barabara kuu akimsimamia punda aliyebeba nafaka (Jumatatu, Novemba 13 mwaka huu) saa 5:10 asubuhi. Mtoto huyo ambaye muda huo alipaswa kuwa dararsani, akawa na ufafanuzi ufuatao:

"Bibi amenituma kwenye mashine kusaga ili tupate unga wa ugali. Leo sijaenda shuleni kwa sababu ninamsaidia kazi bibi."

**JICHO LA CAG**

Kile ambacho Nipashe imeona na kuthibitishwa na wenye dhamana kitaifa katika eneo hilo, pia kimetupiwa jicho na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kufanyiwa tathmini katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka 2020/21.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Charles Kichere anabainisha kuwa, sampuli za halmashauri 27 alizozikagua, inaonesha kuwa kati ya mwaka 2018 na 2021, wanafunzi 18,670 walishindwa kuhitimu elimu ya msingi.

Kwa mujibu wa CAG Kichere, hali ni mbaya zaidi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo kati ya wanafunzi 13,625 waliosajiliwa, 7,565 walikatisha masomo, ikiwa ni zaidi ya nusu (asilimia 55) ya wanafunzi wote waliosajiliwa.

INAENDELEA UK. 5

# TAMWA yakumbusha wazazi umakini malezi ya watoto

**Na Beatrice Moses**

MKURUGENZI Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, amewakumbusha wazazi, walezi na walimu kuongeza umakini kuwalinda watoto wa kike na wa kiume dhidi ya ukatili, kwa kuwa ni hatari kwa taifa lijalo iwapo litakuwa na viongozi waliojeruhiwa kwa kuathirika kimwili na kisaikolojia.

Dk. Rose alisema TAMWA itaendelea kushirikiana na wadau wengine na vyombo mbalimbali vya habari kuibua na kutoa elimu itakayosaidia watoto kuwa salama.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Miaka 36 ya Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

"Tumemkaribisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kuwa mgeni rasmi wa maadhimisho haya, yenye kaulimbiu: 'Uongozi Bora na Mchango wa Wanawake ni Chachu Kuelekea Tanzania Yenye Maendeleo Endelevu', alisema.

Katika maadhimisho hayo yatayofanyika kwa siku mbili kuanzia kesho jijini Dar es Salaam, TAMWA inatarajia kuzindua nakala ya Jarida la Sauti ya Siti, ambalo limeripoti kuhusu rushwa ya ngono katika vyombo vya habari, pia itazindua ripoti ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia ndani ya vyombo vya habari.

Dk. Rose alibainisha kuwa katika maadhimisho hayo pamoja na mambo mengine itatoa tuzo kwa mwanahabari aliyefanya vizuri katika uandishi wa habari za masuala ya afya ya uzazi pia zawadi maalumu kwa waasisi 13 wa chama hicho ikiwa ni alama ya kutambua na kuthamini mchango wao. Maadhimisho hayo yanatarajiwa kupata washiriki wakiwamo wabunge kutoka nchini Kenya na Tanzania, mabalozi na viongozi wa dini na siasa na taasisi za watu binafsi.


Alisema TAMWA ambayo imeendelea kujikita kuhamasisha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto nchini, ikilenga kuona jamii ya kitanzania inayoheshimu haki za binadamu kwa mtazamo wa usawa wa kijinsia.

Akizungumzia mafanikio ya TAMWA katika miaka 36, Dk. Rose alisema ushirikiano mzuri wa ushawishi na wadau wengine ndiyo uliochochea Bunge kutunga Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998 ambayo inazuia ukatili wa kijinsia na kulinda heshima, hadhi, utu na haki za wanawake na watoto.

"Awali mwanamke akipigwa na kujeruhiwa na mume, aliogopa kusema ukweli badala yake alisema ameanguka, mtoto ananajisiwa wanakaa kimya na hata mke akiuawa, wanakaa na kuyamaliza kimya kimya, sasa imekuwa tofauti, wengi wanasema hadi kwenye vyombo vya habari ni wazi wanapinga ukatili wa kijinsia," alisema Dk. Rose.

Mafanikio mengine ni kuongeza idadi ya wanawake viongozi, pia kuondolewa kwa sheria ya wanawali ya mwaka 1985, ambayo msichana akipata mimba alifungwa jela, pia kama ni mwanafunzi hakuruhusiwa kurudi tena kusoma shule.

"Sheria hii iliondolewa kwa jitihada na ushawishi wa Rais Samia, ambaye kwa wakati huo alikuwa Waziri Zanzibar aliyekuwa na dhamana ya masuala ya kijinsia. Na yeye alilibeba tatizo hilo hadi hatimaye ile sheria ikafutwa," alisema..



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, akizungumza na Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC), Aristid Kanje, kuhusu namna chama hicho kitakavyoweza kuchangia katika ujenzi wa CATC wakati wa kikao kilichofanyika katika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya CCM, Lumumba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wilaya ya Bunda na maisha hasi kwa watoto

**Inatoka Uk. 4**

| H/shauri | Andikishwa | Walioacha |
|---|---|---|
| Bunda | 13,625 | 7,565 |
| Tarime | 12,775 | 4,486 |
| Urambo | 8,137 | 4,408 |
| Biharamulo | 9,511 | 3,932 |
| Babati | 14,569 | 3,900 |
| Ushetu | 9,219 | 3,274 |
| Magu | 12,424 | 2,779 |

**Idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo katika baadhi ya halmashauri nchini kati ya mwaka 2018 na 2021. CHANZO: Ripoti ya CAG kuhusu Ukaguzi wa Serikali za Mitaa 2020/21. Uk. 115**

CAG anahitimisha, "Tathmini yangu ilibaini kuwa sababu kuu za kuacha shule kwa wasichana zilihusiana na matukio ya ujauzito ambayo yanatokana na umbali mrefu - toka nyumbani hadi shuleni - asili ya familia na masuala mengine binafsi.

"Sababu zingine ni pamoja na kuhamahama kwa familia zinazojihusisha na ufugaji, maeneo ya kijiografia na uelewa mdogo wa umuhimu wa elimu kwa baadhi ya jamii ambazo sehemu kubwa ya wazazi wanapendelea watoto wao kulima na kuchunga mifugo kuliko kwenda shule," anabainisha.

Kichere anapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine kuwezesha uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu na kuboresha mazingira ya shule hususan vijijini.

Hayo yanaibuliwa wilayani Bunda kipindi ambacho Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimetoa ripoti ya utafiti inayoonesha haki za elimu, afya, chakula, maji safi na salama, mazingira, faragha na familia zimeathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi huku watoto na wanawake wakiathirika zaidi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Dk. Anna Henga, utafiti wao umebaini kundi hilo limeathirika zaidi kutokana na mtindo wa kuhamahama unaofanywa na baadhi ya familia ili kupata mahitaji yao, jambo lililosababisha baadhi ya watoto kutopata haki ya elimu, huku baadhi ya wazazi wakitelekeza familia kutokana na hamahama hiyo.

# Tanzania kushirikiana vyuo vya ufundi China

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeahidi kuingia makubaliano na vyuo 11 vya ufundi nchini China kwa lengo la kubadilishana ujuzi na uzoefu na kuboresha mitaala ya elimu ya ufundi kupitia ushirikiano uliopo wa China-Africa Alliance.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula, alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na ujumbe huo kutoka China katika semina ya siku mbili iliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Stadi (NACTIVET) ya kubadilishana ujuzi na uzoefu na kutafuta maeneo ya kushirikiana.

Alisema Serikali ya Tanzania kwa sasa inaelekeza nguvu kubwa katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi ili kuwapa vijana ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuwa na sifa za kuajiriwa wanapohitimu.

"Wenzetu China wameendelea sana kwenye elimu ya ufundi viwanda vingi vya nchini mwao vinaendeshwa na wataalamu wao wa elimu ya ufundi sasa Watanzania tunataka kujifunza ili na sisi vyuo vyetu vizalishe wataalamu watakaoshindana kitaifa na kimataifa," alisema.

Alisema uhusiano wa Tanzania na vyuo hivyo ulianza muda mrefu na mwezi Aprili, mwaka huu timu ya Watanzania ilitembelea vyuo mbalimbali nchini China kujifunza elimu ya ufundi stadi.

"Kupitia ushirikiano wa China-Africa Alliance, wataalamu wetu wanakutana mara kwa mara kubadilishana uzoefu na huu ni mwendelezo wa juhudi za serikali zilizofanywa kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha vijana wanapata ujuzi wa kisasa utakaowawezesha kushindana kitaifa na kimataifa," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTIVET), Dk. Adolf Rutayuga, alisema kupitia ushirikiano huo wanafunzi wa vyuo vya ufundi nchini watapata nafasi ya kwenda China kujifunza namna elimu hiyo inavyotolewa nchini humo.

"Wanafunzi wa vyuo vya China watakuwa wanakuja Tanzania kwa hiyo tutakuwa tunabadilishana utaalamu kati ya walimu wanaofundisha kwenye vyuo vyetu na tutajifunza wao wanawajengeaje ujuzi wanafunzi wao na tunaamini ushirikiano huu utawapa ujuzi na umahiri vijana wetu na wa kwao," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la NACTIVET, Profesa John Kondoro, alisema ushirikiano huo umejengwa katika kuendeleza mafunzo ya elimu ya ufundi kwa manufaa ya vijana wa nchi hizo mbili.

Alisema kuna kampuni nyingi zinazokuja kufanyakazi nchini na mara nyingi zinapokuja zinakuwa na viwango vya kimataifa na kwamba kuna umuhimu kwa wahitimu wa vyuo nchini kutambua viwango vinavyohitajika kimataifa.

"Vijana wetu wanapaswa kufahamu kwamba China imepiga hatua kubwa sana katika suala la teknolojia kwa hiyo tunaposhirikiana tunataka kuwezesha vijana wetu wapate ujuzi na maarifa ya kushindana katika ngazi ya kitaifa na kimataifa pia," alisema Profesa Kondoro.

Alisema baadhi ya wahitimu nchini wanaweza kuamua kwenda kufanyakazi nje ya nchi ili wakubalike kwenye soko la ajira lazima wawe na viwango vinavyohitajika kwenye mataifa ya nje.

Kwenye ushirikiano huo, vyuo vya China vitaisaidia Tanzania kutengeneza na kuboresha mitaala na viwango vya mafunzo ya umahiri yanayotolewa hapa nchini.

"Kwa wenzetu China mafunzo ya vyuo vya ufundi yanazingatia zaidi umahiri siyo nadharia kwa hiyo tutajifunza namna gani wenzetu wamefanikiwa kujenga umahiri kwa wanafunzi wao na walimu wao ili na sisi tutoe mafunzo yanayokidhi viwango," alisema Profesa Kondoro.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rekodi bado zinazibeba Simba, Yanga robo CAF

**WAWAKILISHI** wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ngazi ya klabu, Simba na Yanga, mwishoni mwa wiki walianza safari yao mpya na ngumu ya hatua ya makundi ya michuano hiyo kwa matokeo yasiyoridhisha sare na kipigo.

Yanga ambayo hii ni mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 25 kucheza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Ijumaa ilianzia ugenini nchini Algeria na kukaribishwa ukubwani kwa kipigo cha mabao 3-0, huku watani zao, Simba wakiwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, wakalazimishwa sare ya bao 1-1.

Hata hivyo, safari bado ni ndefu kwa timu hizo kwani hizo ni mechi za kwanza kati ya sita ambazo zinatakiwa kucheza kusaka tiketi ya kufuzu robo fainali ya michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Kwa Yanga sasa inakabiliwa na mchezo mwingine mgumu zaidi Jumamosi wiki hii, nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Al Ahly ya Misri iliyotoka kushinda mabao 3-0 nyumbani dhidi ya Medeama ya Ghana wakati Simba yenyewe itakuwa ugenini nchini Botswana dhidi ya Jwaneng Galaxy ambayo imetoka kushinda ugenini kwa bao 1-0 dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.

Hata hivyo, tunaamini Simba na Yanga zitajipanga vema kuelekea mechi hizo ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu robo fainali na hatimaye nusu fainali na ikiwezekana fainali kabisa, kwani licha ya matokeo ya kwanza kutoridhisha tunaimani kubwa kwao hasa tukizingatia rekodi zao za msimu uliopita.

Msimu uliopita, Yanga ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ilianza kwa kufungwa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ya Tunisia kabla ya kuibugiza TP Mazembe mabao 3-1 katika mechi iliyofuata, na kisha ilienedelea kushinda hadi kutinga fainali na kuukosa ubingwa dhidi ya USM Alger.

Kama ilivyo kwa Yanga, Simba ikiwa Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, ilianza kwa kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Horoya ya Guinea, kisha ikarejea nyumbani na kupigwa 3-0 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, lakini baada ya hapo ilamka na kuanza kutoa vipigo kikiwamo cha karaha kwa kuibugiza Horoya mabao 7-0 katika mechi ya marudiano na kutinga robo fainali.

Hivyo, tunaamini bado zina nafasi kubwa ya kurekebisha mapungufu yao na kufanya vizuri katika mechi zinazofuata na haitatushangaza kuziona zote zikiandika historia nyingine kwa kutinga robo fainali kwa msimu mmoja kama ambavyo zote zimeingia hatua ya makundi kwa pamoja msimu huu.


Kikubwa kwa Simba na Yanga ni kushuka uwanjani zikiwa na lengo kuu la pointi tatu zaidi badala kuishia kumiliki mpira kwa kutaka kufurahisha mashabiki jukwaani na mwisho wa mchezo wapinzani wao wakibeba alama muhimu.

Lakini pia, huu ni wakati muafaka kwa mashabiki wote wa timu hizo na viongozi, kusimama nyuma ya wachezaji wao kwa kuwasapoti hususan wanapocheza nyumbani ili kuwaongezea maorali wa kufanya vizuri katika mechi zao.

Kwa Yanga ambayo inarejea nyumbani kucheza dhidi ya Al Ahly, pamoja na kuwaheshimu mabingwa hao watetezi wa michuano hiyo, lakini isiwaheshimu hadi kupitiliza, bali ipambane mwanzo mwisho kwa kutambua ni muhimu kuvuna alama katika uwanja wa nyumbani.

Kadhalika, Simba inapaswa sasa kwenda kuokota alama ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy, ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutinga robo fainali, hili linawezekana tu kama kila mchezaji atatambua thamani ya kuaminiwa na kupewa jezi ya klabu yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Simba, Yanga bado zina nafasi kufika robo fainali

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWA** na mashaka mengi kwa timu za Tanzania, Simba na Yanga zinazocheza Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kama zitatoboa robo fainali. Hii ni baada ya kushindwa kupata ushindi katika mechi zao za kwanza zilizocheza.

Ijumaa iliyopita, Yanga ilikuwa ya kwanza kuwanyong'onyesha Watanzania ilipotandikwa mabao 3-0 dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria.

Wakati wakitafakari kipigo hicho, timu nyingine ya Tanzania, Simba ikalazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Asec Mimosas, mechi ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Si kawaida kwa Simba kutoshinda kwenye uwanja huo ambao mara nyingi ndiyo umekuwa ukiwawezesha kutinga robo fainali ya ligi hiyo.

Inaweza isishinde hata mechi moja ugenini, lakini mara nyingi pointi tisa za nyumbani ndizo zinazoivusha.

Pamoja na kwamba hii ni mara ya kwanza kwa timu hizo za Tanzania kwa mara ya kwanza kucheza Ligi ya Mabingwa kwa pamoja, lakini matokeo hayo ya mwanzo yameanza kuwatia wasiwasi mashabiki wa soka nchini.

Tena afadhali kidogo Yanga, ambao wengi wana wasiwasi tu kwa sababu kuna vigogo viwili kwenye kundi lake, Al Ahly na CR Belouizdad kwenye Kundi D, Simba imeanza kukatiwa tamaa mapema hata na mashabiki wake kutokana na kiwango kibovu ambacho imekuwa ikikionesha kwenye mechi za hivi karibuni.

Binafsi, naona mashabiki wa soka na wanachama wa timu hizi mbili na hata wadau, wasianze kuzikatia tamaa kwani ndiyo kwanza ni mechi za kwanza za makundi.

Msimu uliopita, Yanga ilianza kwa kufungwa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ya Tunisia, mechi za Kombe la Shirikisho Afrika, kila mmoja akadhani huenda ikawa ndiyo kibonde wa kundi, lakini kilichotokea ni kwamba baada ya kuitwanga TP Mazembe mabao 3-1 katika mechi iliyofuata, mlolongo wa ushindi ukaanza, ikawa inashinda pia ugenini, hadi kufikia fainali ya michuano hiyo, ambayo bingwa wake akawa ni USM Alger.

Tena Yanga ilishinda mechi ya ugenini nchini Tunisia bao 1-0, kama si kufungwa mabao 2-1 nyumbani, ingeweza kutwaa kombe hilo.

Msimu uliopita kwenye michuano hii hii ya Ligi ya Mabingwa, Simba ilianza kwa kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Horoya ugenini Februari 11, mwaka huu.

Kila mmoja akaona timu ya mwaka huu haiendi popote. Na kama haitoshi, Februari 18 ikabamizwa mabao 3-0 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, hapo sasa wanachama na mashabiki wakaikatia tamaa.

Ikaanza kutoa kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Vipers FC ya Uganda katika mechi zote mbili ya ugenini na nyumbani, ikajikusanyia pointi sita na kuweka hai matumaini.

Mechi iliyotakiwa kushinda dhidi ya Horoya ili kukata tiketi ya kutinga robo fainali, ilifanya hivyo na kuiangamiza mabao 7-0.

Hapa unaweza kuona kuwa pamoja na timu za Tanzania kutoshinda mechi zao, basi wala si sababu ya kudhani au kutabiri kuwa haziwezi kufanya vizuri.

Jwaneng Galaxy ya Botswana imeifunga Wydad Casablanca bao 1-0 mechi ikichezwa nchini Morocco na hiyo inathibitisha kuwa timu yoyote inaweza kushinda mechi popote kama ikijiandaa vema.

Cha kufanya ni kwamba viongozi wa timu hiyo, mabenchi yao ya ufundi na wachezaji wanapaswa kukaa na kuangalia wapi kuna mapungufu ya kuyarekebisha ili kwa mara ya kwanza pia tuone timu zote mbili za Tanzania zikitinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Halmashauri yajivunia kuvuka lengo la makusanyo ya mapato

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibaha imevuka lengo la ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 14, hatua inayotajwa kuongeza chachu katika utekelezaji miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Makala, alisema mwishoni mwa wiki kuwa kazi nzuri imefanyika kwenye makusanyo ya ndani.

Alibainisha kuwa mapato ya kila mwezi ni zaidi ya Sh. bilioni 2.2 na mapato ya ndani pekee ni Sh. bilioni 1.8, hivyo kufikia asilimia 39 na kuvuka lengo kwa zaidi ya asilimia 14.

Alibainisha hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo. Alikumbusha kuwa asilimia 40 ya mapato inatakiwa ielekezwe kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi hususani iliyoibuliwa na kuanzishwa na wananchi na asilimia 60 zitumike katika matumizi ya kawaida. Makala alisema Baraza la Madiwani, halitasita kuchukua hatua dhidi ya watendaji watakaobainika kutoa mianya ya upotevu wa mapato na usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo.

Alisema ni wajibu wa Baraza la Madiwani kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watendaji wazembe na wasiozingatia maadili ya kazi, ikiwamo wanaosababisha upotevu wa mapato ya ndani na usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo.

Diwani wa Kiwawa, Alfred Malega alisema wananchi wanakabiliwa na kero nyingi, hivyo ongezeko la ukusanyaji matapo litasaidia kutekeleza miradi hiyo.

"Tumeongeza makusanyo, ni matumaini yangu kwamba zitatumika kwa mujibu wa utaratibu ambao upo na unafahamika wa asilimia 40 miradi ya maendeleo na asilimia 60 matumizi ya kawaida.

"Tunaona kuna matatizo mengi ya wananchi ambayo yameibuliwa kwenye vikao, sasa yanakwenda kutatuliwa," alisema.

Diwani wa Viti Maalum, Grace Mshindo kutoka Tarafa ya Mlandizi, alisema vikwazo ambavyo vinawakabili wananchi ambavyo vipo nje ya bajeti, vitazamwe na halmashauri hiyo na kutatuliwa ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

## Mbarawa aagiza maboresho ya bandari yakamilike kwa wakati

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, ameitaka Kampuni ya China Railway Major Bridge Enginnering Limited (CRMBEG) kuhakikisha mradi wa maboresho katika Bandari za Bukoba na Kemondo unakamilika Mei mwakani ili meli ya MV. Mwanza itoe huduma katika bandari hizo.

Baada ya kukagua miradi hiyo mkoani Kagera mwishoni mwa wiki, Waziri Mbarawa alisema kukamilika kwake kutarahisisha shughuli za uchukuzi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi jirani. "Ninawapongeza kwa hatua iliyofikiwa, lakini niwakumbushe kuwa ujenzi wa meli ya MV. Mwanza uko katika hatua mbalimbali za kukamilishwa na itakapokamilika itatumia bandari hizi mbili kutoa huduma, hivyo lazima tuongeze kasi ya ujenzi hususani kwenye gati angalau moja kwa kila bandari ili kuruhusu meli yetu ya MV Mwanza kutoa huduma itakapokamilika," aliagiza.

Waziri Mbarawa pia aliitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kuhakikisha vifaa maalum vya kuongozea meli vinawekwa Ziwa Victoria ili huduma zitolewe katika hali ya usalama.

Mkuu wa Wilaya ya Misenyi, Kanali Wilson Sakulo, alishukuru serikali kwa kuendelea kuwekeza fedha katika usafiri majini na miundombinu yake kwa kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kutachochea ukuaji biashara kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mhandisi Mkazi wa Kampuni ya Dar Al Handah Consultants, Joshua Lesha, alimhakikishia Waziri Mbarawa wataongeza kasi ya utekelezaji miradi hiyo miwili kwa kuwa vifaa vya ujenzi karibu vyote vipo kwenye eneo la mradi.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Juma Kijavara, alisema miradi inayohusisha maboresho ya Bandari ya Kemondo na Bukoba umefikia asilimia 25 na mamlaka hiyo itahakikisha inamsimamia mkandarasi ili akamilishe mradi huo kwa wakati.

Mradi wa Bandari ya Kemondo na Bukoba unaohusisha ujenzi wa gati, majengo ya abiria na miundombinu mingine na unatarajiwa kukamilika Mei mwakani kwa gharima Sh. bilioni 40.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasalimia wafanyakazi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) alipotembelea maonesho ya Wiki ya Huduma za Kifedha yaliyomalizika mwishoni mwa wiki jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wagundua teknolojia kuzuia upotevu wa maji

**Na Elizabeth Zaya**

WANASAYANSI chipukizi wanaowezeshwa na Taasisi ya isiyo ya kiserikali ya Young Scientists Tanzania (YST), wamegundua teknolojia mpya ya kuzuia upotevu wa maji katika mifumo ya umwagiliaji.

Mbali na mfumo wa umwagiliaji, vijana hao pia wamegundua namna ya kuweka sawia mtawanyiko wa virutubisho katika udongo, njia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, njia salama za usambazaji maji na kuzuia upotevu wake kwa kutumia vifa maalum vya utambuzi na panya pamoja na matumizi ya nguvu za jua kuondoa taka baharini.

Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema ugunduzi huo umejikita kutatua matatizo katika jamii.

Alisema ugunduzi huo unatarajiwa kuoneshwa katika maonesho ya kitaifa ya YST yatakayofanyika Desemba 5 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Yatajumuisha wanafunzi 90 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

"YST imekuwa ikilea vipaji vya kisayansi miongoni mwa vijana wanaosoma shule za sekondari kwa miaka 13 sasa na imekuwa inatoa fursa kwa vijana hao kupatiwa mafunzo ya mbinu za kiutafiti wa sayansi, kufanya utafiti wa kisayansi na kufanya ugunduzi wao baada ya mchakato mrefu wa kiutafiti," alisema.

Dk. Kamugisha alisema mwaka huu wanafunzi waliotuma maombi ya ugunduzi ni 979, wakiomba fursa ya kushiriki katika programu ya YST na kwamba baada ya kufanya mchujo, maombi 361 yalichaguliwa na wanafunzi wakapatiwa mafunzo namna ya kuendeleza kazi hizo za kisayansi.

Pia alisema ugunduzi bora uliooneshwa kwenye mashindano ya kimkoa umechaguliwa kuwakilisha mikoa yao katika mashindano ya kitaifa yatakayojumuishwa kazi 45 za ugunduzi.

Miongoni mwa wadhamini wakubwa wa maonesho hayo ni Taasisi ya Karimjee Foundation ambayo kupitia kwa mwakilishi wake, Caren Rowland, ilisema mpaka kufikia mwaka jana, imedhamini wanafunzi 41 kusoma vyuo vikuu.

"Karimjee Foundation ina furaha kubwa kuona YST imefikia mikoa yote na shule zote nchini na maono ya taasisi yetu ni kuendeleza kizazi kijacho cha viongozi wanaoleta mabadiliko na wabunifu ambao wanaleta tija kwa Tanzania na dunia kwa ujumla," alisema Caren.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Kampuni za Britam Holdings PLC, Kuria Muchiru (wa pili kulia), akikabidhi zawadi kwa Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Saqware wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 25 ya Kampuni ya Bima ya Britam Tanzania katika soko la bima Tanzania jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatwaa tuzo ya Mlipakodi Mkubwa na Bora Zaidi Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

MWISHONI mwa wiki kwenye Siku ya Mlipakodi 2023, Benki ya NMB iliibuka Mshindi wa Jumla Kitaifa kama Mlipakodi Mkubwa Zaidi Tanzania na kama Mlipakodi Bora Zaidi Anayelipa Kodi kwa Hiari (Most Compliant Tax Payer).

Huu ni mwaka wa pili mfululizo kwa benki hiyo kupata tuzo hizi.

Jumla ya Tuzo ilizopata Benki ya NMB ni: Mshindi wa Jumla Kitaifa: Taasisi Inayolipa Kodi Kubwa Zaidi nchini (sekta zote), Mshindi wa Jumla Kitaifa: Taasisi Bora Inayolipa Kodi kwa Hiari kwa Kuzingatia Misingi na Kanuni Bora za Ulipaji Kodi, Mshindi wa Kwanza: Mlipakodi Mkubwa Zaidi Kundi la Taasisi za Fedha nchini (kwa mara ya tatu mfululizo).

Baada ya kupokea tuzo hizo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna alisema ni matokeo chanya ya misingi imara ya utawala bora na uadilifu, kuzingatia kanuni za ulipaji kodi, ufanisi katika kuendesha biashara na ubunifu wa suluhishi bora za kifedha kwa wateja.

Ruth alisema, "ninawashukuru wateja wetu na Watanzania wote kwa kuendelea kuiamini Benki ya NMB kama mshirika wao kwenye biashara na shughuli zao.

"Ninaishukuru Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya Biashara nchini na kipekee ninawashukuru wafanyakazi wenzangu wote wa Benki ya NMB kwa kuendelea kufanya kazi kwa ari, bidii na kwa uzalendo mkubwa kwa maslahi mapana ya benki na nchi yetu kwa ujumla."

Tuzo hizo za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zilitolewa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko katika hafla iliyofanyika Mlimani City, Dar es Salaam.

Kama mdau wa maendeleo, Ruth alisema Benki ya NMB itaendelea kuendesha biashara kwa kuzingatia sheria na kanuni za nchi ili kuendelea kuchangia kikamilifu ujenzi wa uchumi wa Taifa.

Katika hafla hiyo ya kuwatambua walipakodi bora wa mwaka, Naibu Waziri Mkuu Biteko alisisitiza azma ya serikali kuendeleza mageuzi ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

Ajenda hiyo alisema ni muhimu kuzidi kuwavutia wawekezaji ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato na ulipaji kodi wa hiari kwa ajili ya kupata mapato ya kuliendeleza Taifa.

"Kuwatunuku walipakodi ni suala muhimu kutokana na mchango wao katika maendeleo kwani bila wao rasilimali zinazohitajika kuchangia ukuaji wa uchumi haziwezi kupatikana kikamilifu.

"Hawa ni wadau wakubwa katika ujenzi wa Taifa ambao hawapaswi kukwazwa kwa namna yoyote ile bali kuelimishwa zaidi na kuhudumiwa vizuri katika ulipaji kodi wao na serikali hii inalizingatia hilo kwa karibu sana," alisema.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, aliipongeza TRA kwa kuziendeleza tuzo hizo ilizozianzisha mwaka 2006, akisema kutambua mchango wa walipakodi kunasaidia mamlaka hiyo kutimiza malengo ya ukusanyaji mapato.

# Walia uchakavu wa miundombinu chuoni

**Na Boniface Gideon,** TANGA

UONGOZI wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Mkoa wa Tanga umewaomba wadau wa maendeleo kusaidia kuboresha miundombinu ya chuo hicho ikiwamo madarasa na mitambo ya kujifunzia.

Mkuu wa chuo, Gideon Ole Lairumbe, aliwaomba wadau mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 47 ya chuo hicho iliyoshirikisha wahitimu 268.

Ole Lairumbe alisema chuo hicho kinatoa mafunzo ya ufundi stadi katika fani 14 za muda mrefu na fani zaidi ya 20 za muda mfupi, lakini kinakabiliwa na changamoto za upungufu wa mabweni, hali inayosababisha idadi kubwa ya wanafunzi kukaa nje ya chuo, uchakavu wa vyoo na mifumo ya majitaka. Alizitaja changamoto zingine ni uhaba na uchakavu wa mashine na mitambo ya kujifunzia kwa vitendo, hali inayosababisha kutumia mitambo iliyopitwa na wakati kulinganishwa na teknolojia ya sasa katika soko la ajira.

Mkuu huyo pia aligusia mwitikio mdogo wa wasichana kusomea fani hizo, akiomba jamii kupeleka mabinti kujifunza fani hizo.

"Ukiangalia mwitikio wa watoto wa kike ni mdogo sana kulinganishwa na wavulana. Walianza wanafunzi 301. Kati yao, wavulana walikuwa 184, na wasichana 117, lakini wanafunzi 33 waliacha masomo (wavulana 14) na leo wanafunzi 268 wanahitimu. Kati yao, wasichana ni 99," alisema.

Meneja wa Benki ya NMB Tanga, Elizabeth Chawinga alisema mwitikio mdogo wa mabinti kusomea fani za ufundi stadi si ishara nzuri katika ustawi na usawa wa kijamii, hivyo akawataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuwapeleka mabinti kujifunza fani hizo kwa kuwa zina soko kubwa la ajira kwa sasa.

"Niwaombe wazazi, walezi na jamii kwa ujumla tuwapeleke watoto wa kike kwenye vyuo vya ufundi stadi, huku kuna soko kubwa la ajira; kujiajiri au kuajiriwa na sisi NMB tupo tayari kuwasaidia," alisema Elizabeth.

# Serikali yaipongeza kampuni ya bima kwa kukinga majanga

**Na Halfani Chusi**

KAMISHNA wa Bima nchini, Dk. Baghayo Saqware, ameipongeza kampuni ya bima ya Britam kwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya bima nchini.

Vilevile, ameipongeza kampuni hiyo kwa ushirikiano inaotoa kwa serikali katika kusaidia waathirika wa majanga ya asili na kutoa bima inayolenga kutoa msaada wa haraka. Amesema umekuwa na athari chanya katika juhudi za kitaifa za kukabiliana na majanga.

Kampuni hiyo ya bima imeadhimisha miaka 25 tangu ilipoanzisha ikiwa na dhamira ya kutoa ulinzi na usalama kwa wananchi.

Dk. Saqware amesema juhudi za kampuni hiyo katika kutoa huduma kwa wananchi zimepokewa vyema na serikali kutokana na mafanikio na mchango chanya wa Britam katika kuimarisha sekta ya bima na kutoa huduma bora za kifedha kwa jamii.

Kamishna Saqware, akizungumza wakati wa maadhimisho ya miaka 25 yaliyofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, alisema:

"Kwanza kabisa ninawapongeza Britam Tanzania kwa kuwa kampuni ya bima yenye msimamo wa kimaendeleo ya kujenga na kulinda wananchi wa Tanzania na mali zao.

"Kupitia huduma zenu mnasaidia Watanzania wengi kuepuka majanga yasiyotarajiwa kama vile moto, mafuriko na majanga mengine ambayo kiujumla yanahitaji usaidizi wa bima."

Alisema bidhaa za bima zinazotolewa na Britam zinawezesha wananchi kujilinda na hatari mbalimbali na serikali inatambua mchango huo muhimu unaochochea kukua kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya nchi kiujumla.

Dk. Saqware alifafanua zaidi, akisema, "ushirikiano wa Britam na serikali katika kusaidia waathirika wa majanga ya asili na kutoa bima inayolenga kutoa msaada wa haraka, umekuwa na athari chanya katika juhudi za kitaifa za kukabiliana na majanga."

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Kuria Muchiru alisema, "dhamira hii ya miaka 25 ya kulinda ndoto zako na kukukinga na majanga, itaendelea kuwa kielelezo kwa nchi yetu na kuongeza uelewa kwa Watanzania ili wajue umuhimu wa kuwa na bima zinazowalinda wao na mali zao," alisema. Mbali na utoaji huduma za bima, Britam pia imechangia katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kitaifa.

Kupitia uwekezaji wake na kutoa suluhisho za ubunifu, Mkurugenzi Muchiru alisema kampuni hiyo imesaidia kujenga mazingira bora ya kifedha na kutoa mchango wa moja kwa moja katika maendeleo ya Taifa kupitia miradi ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), barabara ya juu ya Kijazi na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere (JNIA) Terminal III.

Alisema Britam itaendelea kuwa chachu ya maendeleo na usalama wa kifedha nchini na kuhakikisha hilo, wameahidi kuwa wabunifu katika utoaji huduma za bima, ili kila Mtanzania anufaike na huduma hizo.

Kampuni hiyo ilianzishwa mwaka 1998 na wafanyakazi watano, ikawa kampuni ya pili ya bima iliyosajiliwa nchini.

Tangu wakati huo imekua na kujiweka kama mtoaji wa suluhisho la ubunifu na la kina la bima ikijumuisha bima ya magari, afya, usafiri na uhandisi.

Katika maadhimisho hayo, kampuni hiyo ilizindua mpango wa ufadhili wa masomo uliopewa jina la 'Britam Scholarship' ambao kwa kuanzia, utatoa msaada wa kifedha kwa wanafunzi wawili wanaoendelea na masomo ya Bima na Usimamizi wa Vihatarishi.

Muchiru alisema mpango wa ufadhili wa masomo ni ishara ya shukrani na kukuza uwajibikaji wa kijamii kwa lengo la kuboresha ustawi wa watu.

# Wafugaji wakopeshwa vifaranga

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ZAIDI ya wafugaji 30 mkoani hapa wamenufaika na Mradi wa Bulding for Better to Morrow (BBT) baada ya kukopeshwa vifaranga wa kuku 21,000 ili kujikwamua kiuchumi kwa kujiajiri katika sekta ya ufugaji.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akigawa vifaranga 9,000 vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 56 kwa wafugaji hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya fedha ya EFTA, Nicomed Bohay, alisema hatua hiyo ni mkombozi kwa wanawake na vijana wanaojihusisha na sekta hiyo ya ufugaji.

"Fedha hizi ni pamoja na vifaranga, chakula, dawa na usafiri kwa wafugaji wetu ili tunapowakabidhi vifaranga wafuge bila kupata mawazo ya kutafuta chakula na dawa," alisema.

Aisema kabla ya kukopeshwa vifaranga hivyo vinavyozalishwa na kampuni ya uzalishaji vifaranga bora ya Silverlands, wafugaji hayo wamepata mafunzo ya ufugaji kwa siku saba.

"Hawa Silverlands wanaozalisha vifaranga pia wanatoa wataalamu wanaowasaidia wafugaji hawa kuwapa elimu na ushauri kila hatua ya ukuaji wa vifaranga lengo letu ni kuhakikisha mfugaji hapati hasara ili arudishe mkopo wake bila shida," alisema.

Aliwaomba Watanzania kutumia fursa ya mkopo wa vifaranga wanaozalishwa na kampuni hiyo ili kuboresha maisha yao kwa kujiajiri na kujiingizia kipato cha kujikimu na mahitaji yao.

Alisema pamoja na mkopo wa vifaranga hao kwa wafugaji, wanatoa fedha za kuwalisha hadi kuuzwa kama kuku wa nyama.


Aliwaomba wafugaji hao kufuga kwa kufuata ushauri na elimu waliyopatiwa ili warudishe mikopo yao na kuwezesha wafugaji wengine kukopeshwa.

Meneja Masoko wa Silverlands Tanzania, Mwanamvua Ngocho, aliwaomba wafugaji hao waliopata mkopo huo kwa awamu ya kwanza mkoani Arusha kuhakikisha wanafanya vizuri na kurejesha.

"Sisi Silverlands tunazalisha vifaranga bora, tunatoa mafunzo kituo chetu cha uzalishaji mkubwa wa vifaranga hawa kipo mkoani Iringa na tunatoa wataalamu wanaosimama na wafugaji hatua zote za ufugaji... tunaishukuru taasisi ya fedha ya EFTA kwa kufadhili mradi huu," alisema.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha, Daniel Loiruck, aliwataka wafugaji hao kuzingatia mafunzo waliyopatiwa ili wawe wafugaji wakubwa wa kibiashara ndani na nje ya nchi.

Mnufaika wa mradi huo, Neema Rweyemamu, alisema amekopeshwa kuku 500 jana wakati akiwa amepatiwa mafunzo na Silverlands mkoani Iringa ya ufugaji wenye tija.



Ofisa Uhusiano wa Bank of Africa tawi la Arusha, Maulid Mussa (kushoto) na Meneja Huduma za Mawakala, Winnie Mushi (aliyesimama), wakihudumia wateja waliotembelea banda la maonesho la benki hiyo katika maadhimisho ya Wiki ya Kifedha jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilionea Laizer ampongeza Samia

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFANYABIASHARA maarufu wa madini nchini, Bilionea Saninuu Laizer amemsifu Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wachimbaji wa madini ya kufanya shughuli zao bila kubugudhiwa na watumishi wa serikali.

Bilionea huyo alitoa sifa hizo katika Kijiji cha Mundarara Wilaya ya Longido wakati wa ibada ya kimila ya kumwombea Rais Samia kutokana na utendaji kazi wake. "Ninapenda kuwashukuru viongozi wa mila waliongoza ibada ya kimila ya kumwombea heri ili afikie mafanikio katika shughuli zake kiongozi wetu wa nchi Rais Samia kwa kazi nzuri anazofanya," alisema.

Alisema kutokana na kuridhishwa na utendaji kazi wake, viongozi wa kimila walifikisha maombi yao kwa Mwenyezi Mungu kumpatia Dk. Samia kibali cha kuchaguliwa tena mwaka 2025 kuongoza Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Longido, Papa Nakuta, alisema Serikali kwa Mkoa wa Arusha imetoa zaidi ya Shilingi bilioni 14 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Mheshimiwa Rais Samia ameleta miradi mingi sana kwenye mkoa wetu wa Arusha kwa kuwa alitoa zaidi ya Shilingi bilioni 14, kadhalika kwenye vijiji na kata zote za Wilaya ya Longido ameacha alama kwa mambo yaliyofanyika na mwakani tunakwenda kufungua kwa mara ya kwanza shule mpya ya sekondari ya Mundarara chini ya kiongozi wa nchi yetu," alisema.

Alimpongeza Saninuu kwa kujenga uhusiano mzuri na jamii inayomzunguka kwa kutoa msaada pale unapohitajika. Vilevile alimpongeza kwa kuwa mwekezaji mwaminifu kwa kuwa amekuwa akilipa kodi ya serikali kwenye biashara.

Awali Kiongozi wa Mila maarufu kama Laigwanani, Piter Sangeyon, alimpongeza mwekezaji huyo kwa kutoa ajira kwa familia zaidi ya 70 kwenye mgodi wa rubi anaomiliki katika Kijiji cha Mundarara.

"Mwekezaji huyu amekuwa msaada kwa jamii yetu kwa kuwa wananchi wanapokuwa na shida wanapomkimbilia anawasikiliza na kuwasaidia kulingana na uwezo wake," alisema. Mwangalizi wa Makanisa ya FPTC, Daniel Laizer, alisema wamefanya sherehe ya kwanza ya bilionea kutoka katika eneo hilo ambaye kwa asili ya kabila lake ni Mmasai.

# Ummy ataka matibabu ya methadone nchi nzima

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WIZARA ya Afya imetakiwa kuweka mpango wa kuhakikisha matibabu ya methadone yanapatikana katika halmashauri zote 184 nchini ili kuwapunguzia vijana wanaotumia dawa za kulevya adha ya kutembea umbali mrefu kupata huduma hizo kwenye baadhi ya vituo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Waziri Ummy Mwalimu wakati akikabidhi vifaa tiba, vitendea kazi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga-Bombo na kugawa vifaa kwa ajili ya vijana waliokuwa wakipata huduma ya methadone.

Vifaa hivyo vilivyokabidhiwa ni vya ujasiriamali kwa ajili ya waraibu waliomaliza matibabu yao na waliopo katika hatua za mwisho ili wajiajiri watakaporudi kwenye maeneo yao.

"Kwani kuna watu wanatoka Pangani, Handeni, Muheza, Korogwe hao watataka nauli kila siku, wanapata wapi kuja kupata dawa na kurudi jambo ambalo linakuwa ni changamoto kwao, " alisema Ummy.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo, alisema vitawasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali na kuachana na fikra za kurudi kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Vifaa walivyokabidhiwa ni kwa ajili ya kutenegeneza madirisha na milango vyenye thamani ya Shilingi milioni 38 na vyerehani 10 vya Shilingi milioni 48 na watakabidhi mashine mbili za kufyatua matofali zenye thamani ya Sh.milioni 70.

Waziri Ummy alimtaka Meya wa Jiji la Tanga wanapotangaza zabuni mbalimbali, kipaumbele kiwe kwa vijana hao ili kuwainua kiuchumi kwa kushiriki kwenye miradi ya uzalishaji mali, maendeleo na kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema kutokana na uwapo wa maombi ya baadhi yao ya kupatiwa eneo la kuoshea magari, watapeleka mpango huo katika Hospitali ya Bombo, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha Mount Meru na ya Mkoa wa Dodoma mashine za kuoshea magari zenye thamani ya Shilingi milioni 90.

Alisema Desemba mwaka huu wanatarajia kununua vifaa vya saluni za kiume kwa ajili ya kuwapatia vijana wengine ambao wapo kwenye hali nzuri baada ya kupata huduma ya methadone ili nao wajiajiri.

"Ndugu zangu vijana wa Tanga ambao bado hamjaingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya msiingie huko, lakini nafurahi kuna taasisi zinaelimisha vijana wa Tanga, naomba waongeze nguvu katika hili ili kuwaepusha vijana na utumiaji wa dawa za kulevya," alisema.

Alizitaka taasisi hizo ziwafikie vijana kwenye shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuwahamasisha wasijiingize kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

"Tunaomba nyie muwe mabalozi tuwe na mpango wa kupita kwenye shule za msingi na sekondari na tunaandaa mambo mbalimbali kuhakikisha tunatoa elimu kwa wanafunzi," alisema.

Kuhusu ukatishaji wa matibabu kwa waraibu, Ummy aliwataka kuachana tabia hiyo mpaka watakapothibitishiwa na madaktari kuwa afya zao zimetengemaa.

"Msikatishe matibabu mpaka mtakapoambiwa mpo sawa, lakini niwatake vijana waliopo majumbani tuache kujiingiza kwenye matumizi ya dawa hizi, " alisema.

Alisema kukabidhiwa kwa vifaa hivyo inaonyesha namna serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu inavyowajali na kuwathamani wananchi wakiwamo wanyonge.


"Niombe Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga, Abdurhaman Shillow, wakati tunajenga ofisi za kata oda (zabuni) ya kwanza watoe kwa vijana hao ambao leo wanapewa vifaa hivyo ili waweze kujikwamua kiuchumi," alisema.

Awali Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Maulid Surumbu, alimpongeza Rais Samia kwa kuangalia makundi yote kwa namna ya kipekee na Waziri Ummy kwa kumsaidia vizuri kiongozi huyo mkuu wa nchi.

Maulid ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, aliahidi vifaa hivyo vitavyosaidia Hospitali ya Bombo vitatumika kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma ya afya kwa wakazi wa Mkoa wa Tanga.

Sambamba na kukabidhi dawa za tiba asili, alisema ni tangu dunia imeanza, zilikuwa hazipewi kipaumbele kama ilivyo sasa zimekuwa zikitolewa na tiba za kisasa.

Aliipongeza wizara hiyo kwa kuwatambua na kuwathamani wananchi na ana imani kwa miaka ijayo Watanzania watatengeneza dawa zinazofanana na wenzao waliotutangulia.





# Matone yaboresha maisha ya walima mboga vijijini

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKULIMA wa mboga wa vijiji vya Wishiteleja na Dulisi wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wamelishukuru Shirika la Tanzania Christian Refugee Service (TCRS) kwa kuwaondoa katika janga la umaskini kwa kuwawezesha katika kilimo cha umwagiliaji wa njia ya matone na ufugaji wa kuku chotara.

Wakulima hao wanaojihusisha na kilimo cha mboga za majani, nyanya na vitunguu kupitia vikundi, wamewezeshwa kuendesha shughuli zao na TCRS chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Norwegian Church Aid (NCA) waliyasema hayo wakati viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na TCRS wakikagua miradi yao.

Katibu wa Kikundi cha Shirikisho, Yustina Lucas, alisema baada ya kuwezeshwa na TCRS kupitia mafunzo na dhana za kilimo cha umwagiliaji, maisha yao yamebadilika kiuchumi baada ya kuanza kuendesha kilimo muda wote na kuuza mazao yao bila kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Aliiomba serikali kuwekeza katika kilimo hicho kwa kuchimba mabwawa mengi katika maeneo mbalimbali nchini ili wakulima waendeshe kilimo cha uhakika na chenye tija badala ya kutegemea mvua na kuwa na uhakika wa kipato na chakula.

"Kabla ya kuwezeshwa katika kilimo hiki nilikuwa na maisha magumu na nilikuwa naishi kwenye nyumba ya tembe, lakini sasa nimejenga nyumba imara ya bati, na wenzangu wamepata mafanikio makubwa wengine wamenunua viwanja, hakuna maisha ya dhiki na njaa kama zamani," alisema Yustina.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Joseph Swalala, aliwapongeza wakulima hao kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata kupitia kilimo hicho ili wafadhili watakapomaliza muda wao mwakani, waweze kujisimamia na kuitekeleza wenyewe.

Ofisa Umwagiliaji Halmashauri hiyo, Mwinula Mtwangi, alisema kilimo ambacho ni cha uhakika kwa sasa ni umwagiliaji na kuwashauri wananchi ambao wamepata elimu hiyo mashamba hayo yawe darasa la kutoa elimu kwa wengine.

Kiongozi wa Mradi kutoka TCRS, Dk. Oscar Rutenge, alisema mradi huo ulianza mwaka 2020 na wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi kupitia vikundi ya kulima kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya matone na ufugaji wa kuku chotara aina ya sasso.

"Lengo la kutekeleza mradi huu wa kilimo stahimilivu kwa mabadiliko ya tabia nchi ni kukuza uchumi kwa wananchi kupitia kilimo chao cha mboga na ufugaji kuku chotara, ili kuongeza usalama wa chakula, kupunguza njaa na kukuza kipato kwao," alisema Dk. Rutenge.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo hadi mwaka 2024, wamekuwa wakishirikiana na wataalamu wa serikali wakiwamo maofisa kilimo, mifugo, umwagiliaji na maendeleo ya jamii kutoa elimu kwa wananchi na kuiomba serikali isimamie miradi ili iwe endelevu.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mohamed Mtanda, akihutubia washiriki wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya programu ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa ndani yaliyoandaliwa na Mgodi wa Barrick North Mara mjini Tarime mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wafundwa kilimo ajira

**Na Remmy Moka,** SAUT

VIJANA nchini wametakiwa kutumia fursa ya kilimo kuwa ajira kwa kuacha kilimo cha mazoea kujikwamua kiuchumi na kuacha kutegemea ajira serikalini kutokana na ongezeko la wasomi nchini.

Kauli hiyo imetolewa juzi wakati wa kuwajengea uwezo vijana zaidi ya 50 kutoka jijini Mwanza wa namna ya kubadili kilimo kuwa fursa kwa kutafuta masoko chini ya uratibu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na VSO kupitia mradi wa EYEE.

Akizungumza na vijana hao, Ofisa Maendeleo ya Biashara Mwandamizi kutoka TADB, Angelina Nyasambo, alisema kutokana na kilimo kuwa uti wa mgongo wa Taifa, kuna haja ya vijana kuweka nguvu kubwa katika kutangaza na kutafuta masoko mazao wanayozalisha na kuacha kilimo cha mazoea.

Alisema benki hiyo imekuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ambapo kwa kipindi hiki wamejikita kwa vijana ambao wako kwenye vikundi vya ufugaji, kilimo na uchakataji wa vyakula vya mifugo.

"Mara nyingi wamekuwa wakiendesha kilimo kwa kutegemea walanguzi, lakini wanachotakiwa kujua ni kuwa kabla ya kuanza kulima ama kufuga tayari wana soko la uhakika ili biashara zako ziwe endelevu, hivyo tunawapa elimu ya kilimo biashara na elimu ya fedha itakayowasaidia kuwakuza katika kilimo," alisema Nyasambo.

Ofisa Biashara na Mikopo TADB Kanda ya Ziwa, Janneth Urio, alisema mafunzo hayo yamewafikia zaidi ya vijana ya 2,000 nchini na ni endelevu ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.

Baadhi ya vijana walioshiriki mafunzo hayo akiwamo Rafidh Adam kutoka katika Kikundi cha Wanamaendeleo kilichopo Kangae mkoani hapa, alisema elimu waliyopata itawasaidia kubadilisha biashara zao kuwa fursa za ajira kwa kutafuta masoko kabla ya kuanzisha ufugaji au kilimo.

# Waandishi nchi 11 waongezewa weledi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAANDISHI wa habari wa nchi 11 wameongeza weledi katika kazi zao kwa kurahisishiwa upatikanaji tafiti za wataalamu kuhusu hali ya mazingira kuzunguka vyanzo vya maji hususani Ziwa Victoria na Mto Nile.

Waandishi hao kutoka nchi hizo zenye uhusiano na Mto Nile, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kenya, Ethiopia, Eritrea, Sudani Kusini, Sudan na Misri wanaunganishwa na watafiti hao katika jukwaa la NileWell chini ya Taasisi ya Waandishi wa Habari ya InfoNile.

Akizungumza wakati wa warsha ya kutambulisha jukwaa hilo kwa waandishi wa habari nchini mwishoni mwa wiki iliyopita, Mratibu wa InforNile Tanzania, Said Sindo, alisema taasisi hiyo yenye makao yake makuu Uganda imefanya utafiti na kubaini waandishi hao wanatumia muda mrefu kupata tafiti hizo.

"Hii ni kufuatia muda mrefu wanaoutumia waandishi ikiwa ni pamoja na kuwagharimu fedha nyingi kununua tafiti hizo na kudhorotesha uandishi wa habari, hivyo kupitia jukwaa hili watafiti pamoja na waandishi wa habari watapata fursa ya kuweka kazi zao na kusomwa, vilevile watawasiliana moja kwa moja ili kuelekezana katika utumiaji wake," alisema Sindo.

Alisema jukwaa hilo litakuwa chanzo muhimu cha upatikanaji wa tafiti na takwimu za kisayansi ambazo zitawasaidia waandishi wa habari katika uandishi wa habari za mazingira na maji.

Mtafiti wa Mazingira na Jiografia, Dk.Laison Kaganga, alisema jukwaa hilo litasadia kutambulisha tafiti zao haraka katika vyombo vya habari na kuwafanya watendaji kuwajibika ipasavyo katika maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi kwa maslahi ya wananchi na viumbe hai.

Mmoja wa waandishi wa habari walioshiriki katika warsha hiyo, Sharifa Suleiman ambaye ni Katibu wa Jukwaa la Waandishi wa Habari za maji na Uhifadhi wa Mazingira Tanzania, (TAJOWEP), alisema watatumia jukwaa hilo kupata takwimu mbalimbali ili kufanikisha kazi ya uhabarishaji jamii.

"Ili kupata tafiti hizi ilikuwa inachukua muda mrefu wakati mwingine inatulazimu kuzinunua, tulikuwa tukipata zile zilizopitwa na muda, hivyo jukwaa hili litakuwa msaada maradufu kwetu," alisema George Binagi, mwandishi wa habari.

Nipashe
Spotika



MIKEL ARTETA ALIFIKISHA MECHI YA 200 'THE GUNNERS' UK. 14



Bernardo Silva

# NAMBA 8 WATANO BORA EPL KWA SASA

**LONDON, England**

MECHI za mpira wa miguu, wanasema, mara nyingi hushinda au kushindwa katika safu ya kati. Katika mazingira ya Ligi Kuu England (EPL), wachezaji wa kati wanatakiwa kuwa na sura nyingi kwani wanahitaji kuchanganya ustadi, akili na uvumilivu. Namba nane mara nyingi ni injini ya timu, inayobeba jukumu la kukera na majukumu ya ulinzi.

Kuanzia kupanga mashambulizi na uchezaji wa pasi sahihi hadi kuvunja michezo ya wapinzani na kutoa safu ya ulinzi, nambari nane anatarajiwa kuwa kiungo mahiri na aliyekamilika vizuri.

Mafanikio katika nafasi hii yanahitaji ustadi wa kiufundi na uwezo wa kusoma mchezo na kufanya maamuzi ya sekunde huku ukidumisha kiwango cha juu cha utimamu wa mwili. Bila kuchelewa wacha tuangalie namba 8 tano-bora zaidi kwenye EPL kwa sasa...

**#5 Bruno Guimaraes (Newcastle United)**

Bruno Guimaraes amekuwa mmoja wa wachezaji waliosajiliwa na Newcastle United katika siku za hivi karibuni. Kiungo huyo wa kati wa Brazil bila shaka ndiye mchezaji wao muhimu zaidi kwani kunakuwa na tofauti kubwa asipokuwapo uwanjani.

Guimaraes ana uwezo wa kucheza katika nafasi nyingi kwenye eneo la kiungo, lakini amebobea kama namba nane. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kila mara anatazamia kuendeleza mpira na ubunifu wake na sifa za kiufundi zimemfanya kuwa mmoja wa viungo wanaotamaniwa sana kwenye sayari hii.

Amefunga bao moja, kutoa pasi moja ya goli, kutengeneza nafasi mbili kubwa na kutengeneza pasi saba na kurejesha mabao 65 katika mechi 11 alizoichezea Newcastle United hadi sasa msimu huu.

**#4 Enzo Fernandez (Chelsea)**

Enzo Fernandez aligeuza kichwa kwa mara ya kwanza kwa uchezaji wake mzuri sana kwa Argentina kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022. Chelsea ilimfanya kuwa mchezaji wao wa bei ghali zaidi kuwahi kusajiliwa wakati wote Januari 2023. Enzo alijiunga na kikosi cha Chelsea ambacho kilikuwa kinachechemea na bado alisimama vema na kiwango chake katika nusu ya mwisho ya msimu wa 2022-23.

Tayari ameshacheza katika nafasi mbalimbali za kiungo kwa Chelsea. Isingekuwa vigumu sana kwa Mauricio Pochettino kufahamu kwamba uwezo wa Fernandez pande zote mbili za uwanja unaweza kuwa muhimu kwa upande wake. Ana kiwango cha mafanikio cha asilimia 56 kwenye Ligi Kuu. Fernandez pia ametengeneza nafasi tatu kubwa kwa upande wake msimu huu.

**#3 Declan Rice (Arsenal)**

Declan Rice ndiye mchezaji aliyevunja rekodi katika Klabu ya Arsenal msimu huu wa majira ya joto walipomsajili kutoka West Ham United kwa kitita cha euro milioni 116.6. Rice alionesha kiwango kizuri katika siku zake za mwanzo akiwa Arsenal ambapo amekuwa akitumika juu zaidi uwanjani.

Huku Thomas Partey akifanya usafi nyuma yake kwenye safu ya kiungo, Rice amepewa uhuru wa kucheza mbele. Nafasi yake bora inaweza kuwa kama kiungo mkabaji, lakini Muingereza huyo mchanga amefanya kazi ya kupongezwa kama namba tisa msimu huu.

Rice amefunga mabao mawili na asisti, alitengeneza nafasi mbili kubwa, ameshinda asilimia 54 ya mashambulizi yake, ameokoa mabao 60 na kufunga mabao 16 katika mechi 12 za Ligi Kuu hadi sasa.

**#2 Dominik Szoboszlai (Liverpool)**

Mashabiki wa Liverpool walikuwa na shauku ya kuona jinsi usajili wao wa bei ghali zaidi kutoka msimu huu wa majira ya joto, Dominik Szoboszlai, utakavyokuwa kwenye Ligi Kuu. Ikiwa kiwango chake katika hatua za mwanzo za msimu mpya ni kitu cha kupita, mashabiki wa Liverpool wanapumzika kwa urahisi wakijua ana mustakabali mzuri pale Merseyside.

Szoboszlai amekuwa na ustadi mkubwa kwa upande wa Jurgen Klopp, akiendeleza mpira vizuri kutokana na ustadi wake mzuri wa kupiga chenga na uwezo wake wa kupiga pasi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hungary pia ni kiungo wa moja kwa moja uwanjani na ni kiungo wa kati ambaye hashindwi kufanya mabadiliko yanayofaa.

Katika mechi 12 za Ligi Kuu akiwa na Liverpool hadi sasa msimu huu, amefunga bao moja na kutoa asisti mbili. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, pia ametengeneza nafasi nne kubwa, alifunga mara 10, akaokoa mara 88 na kushinda asilimia 71 ya mashambulizi yake.

**#1 Bernardo Silva (Manchester City)**

Bernardo Silva amerejea kwenye ubora wake msimu huu. Licha ya kuwa si kielelezo halisi, Silva ni mtu mgumu katika safu ya kiungo. Ingawa yeye ni mbunifu zaidi, yuko kwenye wito kila wakati kutekeleza majukumu yake ya ulinzi pia.

Silva amekuwa muundaji mkuu wa Manchester City katika hatua za mwanzo za msimu wa 2023-24 bila Kevin De Bruyne. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amefunga mabao matatu na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi tisa za Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu.

Pia ametengeneza nafasi kubwa, akarejesha mabao 24 na kushinda asilimia 55 ya makabiliano yake hadi sasa msimu huu.

## ISIKUPITE

ERLING Haaland hajavunja tu rekodi, ameivunja na kuwa mshambuliaji mdogo, akitumia mechi 48 tu za ligi kufikisha mabao 50 kwenye Ligi Kuu England. Idadi hiyo inamfanya kuwa kinara wa kufunga mabao mengi zaidi katika ligi tano bora Ulaya - Premier League, Serie A, Bundesliga, La Liga n Ligue 1, tangu kuanza kwa msimu uliopita. Pia mabao yake 50 katika mechi 48 yanamweka mbele ya Harry Kane, ambaye amefunga mabao 48 katika mechi 50 za Tottenham na Bayern Munich.



## Extra Time

# WANASOKA WATANO MATAJIRI ZAIDI DUNIANI MWAKA 2023



BOLKIAH

**LONDON,** England

WAKATI kulikuwa na zaidi ya watazamaji bilioni tano katika mashindano ya Kombe la Dunia la FIFA 2022 nchini Qatar, mpira wa miguu unabakia kuwa ndio chaguo namba moja kwa michezo mingi iliyopo kwenye sayari hii.

Ingawa "mchezo huu mzuri" ni burudani tu kwa wengi, wengine si tu wamejipatia riziki bali pia wamejikusanyia mali na kuwa wanasoka matajiri zaidi duniani.

Huku wengine wakipata utajiri wao kupitia mikataba ya kuidhinishwa na uwekezaji pamoja na mishahara yao, makala haya yanaorodhesha wachezaji wa kandanda wenye utajiri zaidi duniani kote katika nchi na ligi mbalimbali.

Ingawa kucheza kamari kwa kutumia baadhi ya tovuti bora zaidi za utabiri wa soka duniani ni njia iliyojaribiwa ili kupata utajiri katika soka, ni imani yao kwamba wanaweza kufikia kilele cha fedha kilichotajwa katika makala haya.

Mara kwa mara thamani ya wachezaji inabadilika kadri muda unavyopita, sasa hii ni orodha ya wanasoka matajiri zaidi duniani kwa sasa...

**1. Faiq Bolkiah - Thamani halisi: Dola Bilioni 20**

Akiwa na wastani wa utajiri wa takriban dola bilioni 20, Faiq Bolkiah ndiye mwanasoka tajiri zaidi wa wakati wote. Akiwa mrithi wa familia ya kifalme ya Brunei, utajiri wake unatokana na hifadhi kubwa ya mafuta ya nchi hiyo.

Brunei, taifa dogo, lenye utajiri wa mafuta katika kisiwa cha Borneo Kusinimashariki mwa Asia, na mojawapo ya nchi tajiri zaidi duniani kwa kila mtu. Na mjomba wa Faiq, Hassanal Bolkiah, ni mmoja wa watu tajiri zaidi duniani, na pia ni kama Sultan wake.

Faiq Bolkiah ameweza kutumia utajiri wa familia yake kusaka mafanikio kwenye soka la kulipwa na kuwa mwanasoka tajiri zaidi duniani. Familia yake inajulikana sana kwa kutumia fedha nyingi kwa bidhaa za kifahari na mali zisizohamishika.

**2. Mathieu Flamini - Thamani halisi: Dola Bilioni 12.6**

Akijivunia kipaji chake cha kucheza katika klabu kadhaa maarufu za soka, zikiwamo Arsenal, AC Milan, na Marseille, Mathieu Flamini, ndiye mwanasoka wa pili kwa utajiri duniani. Licha ya kupata fidia kubwa na motisha kama mchezaji na pengine kupata mapato makubwa kutokana na uidhinishaji na mikataba ya udhamini, utajiri wa Flamini hautokani tu na taaluma yake kama mwanasoka.

Flamini aliweka msingi wa kuwa mmoja wa wanasoka tajiri zaidi duniani mwaka 2008 kwa kuwa mwanzilishi mwenza wa Kampuni ya Kemikali ya GFBiochemicals na mshirika wake wa kibiashara, Pasquale Granata.

GFBiochemicals ni kampuni inayojishughulisha na utengenezaji wa kemikali ya asidi ya levulinic. Kemikali hii inatumiwa katika dawa, chakula na vipodozi.

GFBiochemicals imewekeza kwa kiasi kikubwa katika utafiti na maendeleo ili kutambulisha asidi ya levulinic sokoni kama mbadala wa kemikali za petroli.

Kampuni ya Flamini ndiyo watengenezaji wa kwanza duniani wa asidi ya levulinic.

**3. Cristiano Ronaldo - Thamani halisi: Dola Milioni 600**

Cristiano Ronaldo, mwanamichezo wa kwanza wa timu ya michezo kuingiza zaidi ya dola za Marekani bilioni moja katika mapato ya kazi (kabla ya kodi), ndiye mwanasoka wa tatu tajiri zaidi duniani.

Katika kipindi chote cha umiliki wake, gwiji huyo wa Ureno amepata mamilioni ya dola za mshahara, fidia na makubaliano ya kuidhinisha baada ya kuzichezea baadhi ya klabu maarufu duniani, zikiwamo Manchester United, Real Madrid na Juventus.

Ronaldo aligonga vichwa vya habari mwaka 2016 aliposaini mkataba wa maisha na Kampuni ya Nike wa dola bilioni moja na kuwa mwanamichezo wa tatu baada ya nyota wa NBA, Michael Jordan na LeBron James kusaini makubaliano hayo ya maisha na kampuni hiyo.

Mbali na makundi makubwa, Ronaldo ndiye mwanamichezo anayelipwa fedha nyingi zaidi katika historia, kwani mkataba wake na Klabu ya Saudia ya Al Nasr, unamhakikishia mshahara wa dola milioni 215 kwa mwaka.

Mbali na kuwa mmoja wa wanasoka tajiri zaidi duniani, Ronaldo pia ni mmoja wa wanamichezo wanaouzika zaidi duniani akiwa ameingiza mamilioni ya dola katika mapato ya ziada kupitia mikataba yenye faida kubwa na makampuni kama vile Nike, Coca-Cola, na Tag Heuer.

Uwekezaji wake katika makampuni kadhaa ya kibiashara, ikiwa ni pamoja na lebo yake ya mavazi, na msururu wa hoteli, pia umechangia hadhi yake kama mmoja wa wanasoka tajiri zaidi duniani.

Ronaldo ni mmoja wa watu wanaofuatiliwa zaidi kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii, akiwa na wafuasi zaidi ya milioni 600. Hii imesababisha makubaliano ya ziada ya uidhinishaji na fursa za mapato, huku nguli huyo wa soka akipata dola milioni 2.44 kwa kila chapisho lililowekwa kwenye ukurasa wake wa Instagram, kiasi ambacho ni kikubwa zaidi kwenye mtandao huo.

**4. Lionel Messi - Thamani ya Halisi: Dola Milioni 550**

Anayechukuliwa kama ndiye mchezaji bora wa kandanda wa wakati wote, uwezo wa ajabu uwanjani, na ufadhili unamweka kama mwanasoka wa nne tajiri zaidi duniani.

Katika maisha yake yote ya soka, raia huyo wa Argentina ameshinda mataji na tuzo nyingi, zikiwamo tuzo nane za Ballon d'Or, tuzo ya mtu binafsi yenye hadhi kubwa zaidi katika soka, na Kombe la Dunia, tuzo ya timu yenye hadhi kubwa zaidi kwenye mchezo wa soka duniani.

Messi ni mmoja wa wanasoka tajiri zaidi duniani kutokana na makubaliano yake ya mikataba binafsi na Makampuni ya Adidas, Pepsi na Huawei, miongoni mwa mengi. Kwa kuongezea, amejitokeza katika matangazo ya chapa kama vile Gillette, Tata Motors, na Mastercard, ambazo zimempatia mamilioni ya dola.

Mikataba ya klabu ya soka ya Messi, pamoja na mapato yake kutokana na uidhinishaji, imekuwa na faida kubwa sana. Mwaka 2017 alitia wino mkataba wenye thamani ya zaidi ya milioni 600 FC Barcelona, na kumfanya kuwa mmoja wa wanamichezo anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani.

Kwa mujibu wa Jarida la Forbes, alikuwa mwanamichezo aliyelipwa fedha nyingi zaidi mwaka 2022 baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili na Paris Saint-Germain (PSG) unaoripotiwa kuwa na thamani ya zaidi ya dola milioni 41 kwa mwaka.

Baada ya ushindi wake wa kwanza wa Kombe la Dunia 2022, Messi alivunja rekodi ya chapisho la kwenye mtandao wa kijamii lililopendwa zaidi katika historia ya dunia hii.

Gwiji huyo wa Barcelona ana machapisho matatu kati ya matano maarufu zaidi ya wakati wote kwenye mtandao wa Instagram.

**5. David Beckham - Thamani halisi: Dola Milioni 400**

Akiwa na mafanikio makubwa na kujulikana ndani na nje ya uwanja, David Beckham ndiye mwanasoka wa tano tajiri zaidi duniani. Muingereza huyo alifurahia maisha mazuri akichezea klabu kubwa kama vile Manchester United, Real Madrid, AC Milan, PSG na Los Angeles Galaxy.

Beckham alikuwa mmoja wa wanasoka wanaolipwa fedha nyingi zaidi wakati wote kutokana na kipaji chake na mafanikio uwanjani, ambayo yalimpa mikataba mizuri.

Beckham ni mmoja wa wanamichezo wanaouzika zaidi duniani kutokana na mwonekano wake wa kuvutia na sura ya haiba, na amefurahia makubaliano ya kuidhinishwa na chapa bora kama vile Adidas, Armani, H&M, na Pepsi.

Ndoa yake na Victoria, nyota wa zamani wa kundi la muziki la Spice Girl, imempa umaarufu na uhusiano zaidi na tasnia ya mitindo, kwani ana chapa yake mwenyewe ya ubunifu wa mavazi.

Akiwa mmoja wa wanasoka tajiri zaidi duniani, Beckham anamiliki chapa yake ya manukato na ameshirikiana na makampuni mengi kutambulisha bidhaa mbalimbali, kuanzia whisky hadi nguo.

Beckham ni mfanyabiashara mwerevu ambaye amewekeza katika biashara mbalimbali za soka, ikiwa ni pamoja na Inter Miami FC, Chuo cha Soka cha London, na Salford City FC.

Aidha, ana ushirikiano na wakala wa kimataifa wa michezo na burudani Global Brands Group kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa chapa yake na maslahi ya kibiashara.

Kwa miaka mingi, Beckham amewekeza katika mali nyingi, ikiwa ni pamoja na makazi ya kifahari huko London, Los Angeles na Miami. Pia ameshirikiana na watengenezaji mali kadhaa kuanzisha biashara mpya zenye faida kubwa, na kuimarisha nafasi yake kama mmoja wa wanasoka tajiri zaidi duniani.

## Nukuu

"Nadhani atakuwa mgumu sana kuondoka Aston Villa. Kwa jinsi wanavyokwenda na mwelekeo Unai Emery anachukua klabuni hapo, ni wapinzani wa kuwania nafasi ya kucheza michuano ya Ulaya tena msimu huu. Kama wanaweza kushindana pande zote mbili. bado hajaonekana. Atakuwa usajili mzuri na nyongeza nzuri kwenye kikosi cha Arsenal," **Kipa wa zamani wa Tottenham Hotspur, Paul Robinson, akiitaka Arsenal kumsajili kiungo wa Aston Villa, Douglas Luiz na kumwanzisha badala ya Kai Havertz.**




"Hisia zangu ni kwamba kuna uwezekano wa asilimia 50 kwamba Leo Messi atarejea Barca. Nadhani Leo anapaswa kustaafu Barca. Barcelona ni nyumbani kwake, lazima amalize soka lake hapa. Ikiwa rais Laporta atachukua hatua hiyo, nadhani. Kurejea kwa Messi Barcelona kutakuja karibu zaidi," **Mshambuliaji wa zamani wa Manchester City na Barcelona, Sergio Aguero.**




"Lakini ilikuwa rahisi sana kwa jinsi tulivyoruhusu na jinsi tulivyokuwa laini katika kila changamoto. Sawa, sisi ni vijana kama timu, lakini hatuwezi kupoteza aina hii ya nafasi ya kuonyesha ubora wetu," **Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, akionesha kukasirika na kuhudhunishwa kwa namna walivyopoteza kwa mabao 4-1 dhidi ya Newcastle United juzi.**



"Lakini ilikuwa rahisi sana kwa jinsi tulivyoruhusu na jinsi tulivyokuwa laini katika kila changamoto. Sawa, sisi ni vijana kama timu, lakini hatuwezi kupoteza aina hii ya nafasi ya kuonyesha ubora wetu," **Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, akionesha kukasirika na kuhudhunishwa kwa namna walivyopoteza kwa mabao 4-1 dhidi ya Newcastle United juzi.**

Ukurasa 13

# REKODI 5 SIMBA, YANGA ZIKIANZA VIBAYA CAF



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, akishangilia bao lake alilofunga kwa mkwaju wa penalti katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi dhidi ya Asec Mimosas, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

HAIKUWA wiki nzuri kwa wanachama na mashabiki wa klabu kongwe mbili za Simba na Yanga zikianza vibaya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ijumaa iliyopita, Uwanja wa Julai 5, 1962 (Stade du 5 Juillet) jijini Algiers, Yanga ilipata kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria katika mechi ya Kundi D, huku Simba ikilazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye uwanja wake wa nyumbani, Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, ukiwa ni mchezo wa Kundi B.

Yalikuwa ni mabao ya Abdelraout Benguit dakika ya 10, Abderrahmane Meziane dakika ya 45 na Lamin Jallow, dakika za nyongeza kabla ya mechi kumalizika, yakiifanya Yanga kuanza vibaya michuano hiyo.

Kesho yake Jumamosi, Pokou Serge aliifungia Asec Mimosas bao dakika 12 kabla ya mechi kumalizika, ambapo Simba ilitangulia kwa bao la Saido Ntibazonkiza alilolifunga kwa mkwaju wa penalti.

Matokeo ya mechi zote mbili yametengeneza rekodi kwa timu hizo ambazo ni hizi hapa...

**Yanga yaanzia ilipoishia**

Mara ya mwisho Yanga kucheza michuano hiyo ilikuwa ni Novemba 8, 1998 dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast na ikapoteza kwa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Baada ya miaka 25 kupita bila kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, Yanga imerejea tena kwenye hatua hiyo, lakini katika mechi ya kwanza tu, ikakutana na kipigo kile kile cha mabao 3-0, hivyo kuanzia ilipoishia.

**Simba sare makundi baada ya miaka 20**

Simba imetoa sare kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi baada ya miaka 20.

Mara ya mwisho kwa timu hiyo kufanya hivyo ilikuwa ni Septemba 7, 2003 ilipotoka suluhu dhidi ya Ismailia ya Misri mwaka huo, ikiingia kwa mara ya kwanza.

Kwa msimu yote minne ambayo Simba imecheza Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi katika mechi za nyumbani, ilikuwa ikishinda na kufungwa.

Michezo ambayo Simba ilikuwa ikitoa sare ni ya hatua za awali na robo fainali za michuano hiyo.

Mfano ni suluhu dhidi ya TP Mazembe Aprili 6, 2019 na dhidi ya UD Songo ya Msumbiji ya Agosti 10, 2019.

**Yanga haijawahi kushinda makundi**

Kipigo cha mabao 3-0 ilichokipata Yanga dhidi ya CR Belouizdad, kimeifanya kuendelea kuwa na rekodi ya kutoshinda mechi yoyote ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi mpaka sasa.

Mara ya kwanza ambayo Yanga ilitinga kwenye hatua hiyo mwaka 1998, ikiwa Kundi B na timu za Asec Mimosas ya Ivory Coast, Manning Rangers ya Afrika Kusini, na Raja Casablanca ya Morocco, Yanga ilicheza mechi sita, ikitoa sare mbili na kupoteza michezo minne.

Ukichanganya na mechi ya Ijumaa iliyopita inakuwa ya saba ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kwa timu hiyo kucheza bila kupata ushindi wowote.

**Mashabiki Simba wachache uwanjani**

Imezoeleka inapocheza Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa mechi za CAF, mashabiki wa timu hiyo huupamba uwanja kwa kuujaza kwa rangi nyekundu na nyeupe kwa kuuzunguka.

Hata Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), wanawafahamu mashabiki wa Simba ni watu wa aina gani linapokuja suala la kujaza uwanja.

Katika mechi ya Jumamosi haikuwa hivyo. Ukiondoa upande wa Magharibi, pande zote zilizobaki zilikuwa na mapengo.

Na hii imesababishwa na mashabiki wengi kutokuwa na imani na kikosi chao hasa jinsi kinavyocheza, lakini pia wakiamini viongozi wao hawawajibiki ipasavyo, hivyo wengi wao kukosa hamu ya kwenda uwanjani.

**Yanga 'pepa' limejirudia**

Kama ilivyokuwa msimu uliopita kwenye hatua ya Makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Yanga imepoteza tena mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Msimu uliopita, ikicheza Kombe la Shirikisho Afrika, ilianza vibaya kwa kuchapwa mabao 2-0 ugenini dhidi ya US Monastir ya Tunisia, mechi ikichezwa Februari 12, mwaka huu.

Baada ya hapo kilichogeuka ni historia kwani ilikwenda moja kwa moja hadi hatua ya fainali.

Rekodi hiyo ndiyo inayowapa matumaini na kutojali sana kupoteza mechi kwa mabao 3-0 dhidi ya CR Belouizdad.

Wenyewe wanaamini kuwa rekodi inaweza kujirudia, huku Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, akisema kuwa 'pepa' limejirudia, akiwa na maana mtihani umejirudia kama ule wa mwaka jana.

## JE, WAJUA?



WAKATI Arsenal ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Brentford juzi, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mikel Arteta, naye alifikisha mechi ya 200 kuwaongoza 'The Gunners' hao. Pia hilo lilikuwa bao la kwanza kwa Kai Havertz kufunga moja kwa moja (lakini la pili) tangu ajiunge nayo kwa pauni milioni 62 majira ya joto. Havertz bao lake la kwanza lilikuwa la penalti dhidi ya Bournemouth Septemba mwaka huu wakati Arsenal ikishinda 4-0.



# Idadi vifo watoto wachanga yashtua

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, amewaagiza watoa huduma za afya kuweka mikakati ya kupunguza vifo vya wajawazito vinavyotokana na uzazi mkoani hapo.

Dk. Mganga alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha wataalamu wa afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida kutokana na takwimu kuonyesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka huu, vifo vya watoto wachanga 416 vimeripotiwa kutokea mkoani hapo.

Akizungumza katika kikao cha kujadili kuhusu vifo vya wajawazito na watoto wachanga mkoani hapa, alisema takwimu za vifo vya watoto wachanga zinaonyesha kukua kwa kila robo mwaka, hivyo kuna haja watoa huduma hao kuweka mikakati madhubuti itakayosaidia kupunguza vifo hivyo.

Dk. Mganga alisema serikali imebaini kuwa vifo vya wajawazito vinaweza kuzuilika na ndiyo maana imeendelea kuboresha mazingira ya sekta ya afya nchini kwa kutoa vitendea kazi, dawa na wataalamu ili watoe huduma bora kwa jamii.

Alisema waganga wakuu wa wilaya wanapaswa kuwa mabalozi wazuri kwa jamii wanazozihudumia kwa kusukuma ajenda za ujenzi wa zahanati kwenye maeneo yao ili kuharakisha huduma za mama na mtoto.

Dk. Mganga alisema zahanati na vituo vya afya vikiwa karibu na wananchi, wajawazito wengi zaidi watajifungua kwa usalama zaidi badala ya nyumbani.

"Timu za uangalizi za mkoa na wilaya fanyeni kazi kwa weledi zaidi ili kubaini changamoto za afya ya mama na mtoto na kuzipatia ufumbuzi kwa wakati, tukumbuke afya bora ya uzazi na mtoto ni msingi wa maendeleo ya taifa lolote na hasa la Tanzania," alisema. Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Ludovick, alisema pamoja na vifo vinavyotokea serikali imeendelea kuboresha mazingira yao ya kazi na huduma za afya kwa wananchi.





Mfanyakazi wa Maabara ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Kitengo cha Damu Salama, Aziza Khamis (aliyevaa unifomu), akiwahudumia wafanyakazi wa taasisi inayojihusisha na utoaji wa misaada kwa wanajamii (RYTHM) walioamua kuchangia damu kwa hiari yao jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Serikali yapania kuleta mageuzi ya kilimo nchini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa kilimo na taasisi ya kuboresha Mifumo ya Masoko katika Kilimo (AMDT) ili kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao wa Wizara ya Kilimo, Enock Nyasebwa, wakati akifungua kongamano la wadau wa kilimo nchini jijini hapa.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali itakuwa inaongoza mageuzi na kupata maoni na mipango kwa kushirikiana na wadau wa kilimo badala ya kufanya mambo yote pekee yake.

"Tunaamini katika sekta binafsi kwa upande wa mitaji kwa sababu kila upande una fursa na changamoto zake, lakini pia kwa kutambua kilimo kwa muda mrefu tumekuwa tukielekea katika kilimo cha kujikimu na kilimo biashara, " alisema.

Alisema serikali inatekeleza pia vipaumbele vitano ambavyo vitasaidia kilimo kuwa biashara na kuvitaja baadhi ambavyo ni tija katika eneo la umwagiliaji.

Alisema lengo ni kuongeza ajira zenye staha hususani kwa wanawake na vijana ambao wanatakiwa kuongezewa thamani ya masoko nje na ndani ya nchi.

Pia alisema serikali itahakikisha inaendelea kutatua changamoto zilizopo katika sekta hiyo ili kumwezesha mkulima kupata bei kulingana na uwekezaji wake.

Mjumbe wa Bodi ya AMDT, Anderson Mlabwa, alisisitiza kuwa taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na wizara katika vipaumbele vyote ili kuhakikisha kilimo biashara kinakidhi sera ya serikali.

# 'Vijana changamkieni kilimo ni utajiri'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka vijana kuchangamkia fursa za kilimo biashara ili kujikwamua kiuchumi, kuongeza pato la taifa na kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

Senyamule alitoa wito huo jijini hapa wakati akifunga kongamano la siku tatu la kujenga uelewa na kubadilishana uzoefu kwa wadau wa kilimo lililoandaliwa na Taasisi ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko katika Kilimo (AMDT).

Alisema kulikuwa na dhana potofu iliyojengeka katika jamii kuwa wanaojishughulisha na kilimo ni watu maskini, lakini ukweli ni kwamba kutokana na mapinduzi yaliyofanyika katika sekta hiyo kilimo ni utajiri.

"Katika hizi siku tatu mlizokaa hapa mtoke na maazimio ambayo yatawawezesha wananchi wetu wanaojihusisha na shughuli za kilimo kuwa na uratibu wa pamoja," alisema na kuongeza kuwa:

"Tunataka kundi kubwa la vijana liingie katika kilimo kwa sababu huko kuna utajiri, watainua vipato vyao, wataongeza pato la taifa na kutatua changamoto ya ajira kwa sababu watajiajiri na kuajiri."

Senyamule alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza nguvu kubwa katika sekta ya kilimo nchini na kuibadili kuwa chanzo kikubwa cha uchumi wa Mtanzania.

"Namshukuru Rais Samia kwa sababu ya utashi wake ambao unafanya sekta ya kilimo inaendelea kuimarika siku hadi siku. Watu walikuwa wakiongelea kilimo kwa dhana ya umaskini lakini sasa kila mtu anatamani kufanya kilimo kwani utajiri uko huko," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa AMDT, Charles Ogutu, alisema kongamano hilo limewashirikisha wadau wa sekta za maendeleo kujifunza na kubadilisha uzoefu na wadau wa kukopesha fedha na vifaa kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kuinuka na kukifanya kilimo kuwa chenye tija.

"Wadau wamekubaliana kuwa na mikakati ya kujisimamia wenyewe kwa sababu tunamini kuwa tunaweza kufanya mambo makubwa zaidi. Baada ya kutoka hapa kila mtu atatumia kile alichojifunza na kuingiza katika mpango mkakati wake," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa AMDT, Dk. Mary Shetto, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wamewafikia wakulima zaidi ya 100,000 nchini.

Alisema wameweka kipaumbele katika uzalishaji wa zao la alizeti kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

"Lengo la kuweka nguvu kubwa katika uzalishaji wa alizeti ni kuunga mkono jitihada za serikali za kuongeza uzalishaji wa zao hilo ili kukidhi mahitaji na kuepuka uagizaji wa mafuta nje ya nchi," alisema.



# RC kuwacharaza viboko wazazi, walezi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ameonya kuwa atatoa adhabu ya kucharazwa viboko mzazi na mlezi atakayekaidi kumpeleka mtoto shule alichechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani kwa kumtorosha na kumwozesha.

Mtaka alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Kambarage Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Alisema hakuna mzazi au mlezi ambaye atabaki salama kwa kupokonya haki ya mtoto kwenda shule.

"Una mtoto amefaulu kwenda kidato cha kwanza muache akasome Mungu atamwamulia kwa njia yake, mwaka huu mtapiga hata deki, ole wenu msipeleke watoto shule, " alionya Mtaka.

Alisema kama mwanafunzi atakuwa amefaulu na kukosa sare, anapaswa kuwa shule ili akapate elimu wakati jitihada za kutafuta nguo hizo za shule zikiendelea.

"Tumesema mtoto aende hata kama hana sare wasamalia wema wapo tutawaomba watawanunulia, sasa wewe ufanye ujinga wako mtoto amefaulu hama Njombe tafuta mkoa wa kwenda," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alisema hatawavumilia wazazi wenye tabia ya kuwapeleka watoto mjini kufanya kazi za ndani wakati wanatakiwa kumuacha apate elimu kwa kuwa ni msingi wa maisha yao ya baadaye.

"Umri huu wa darasa la saba mtoto anaenda kuwa mfanyakazi kwa nani? Njombe hakuna kiwanda cha wafanyakazi wa ndani, watoto wote waende shule," alisema Mtaka.

Kwa upande wao wazazi akiwamo, Mashaka Lulambo, alisema hakuna mzazi ambaye anashindwa kumwandalia mtoto sare za shule bali wapo wanaofanya makusudi.

"Mimi naamini hakuna mzazi ambaye anashindwa kumwandalia mtoto wake sare kwa sababu wakati fulani hata mtoto wako akiwa yupo na mwenzie na hana sare tayari kisaikolojia mtoto anakuwa ameathirika maana yake anajiona yuko tofauti na mwenzie," alisema Lulambo.

Alisema ni vema wazazi wakachukua jukumu la kuandaa sare mapema kabla ya siku za Krismasi na Mwaka Mpya ili kupunguza majukumu.

Husna Masoud, alisema kuna wimbi kubwa la watoto wanaozurura mitaani bila ya kwenda shule na wanapoulizwa wanadai wazazi hawana fedha.

"Wako wazazi wanakwenda mitaani kunywa pombe wana hela kumpeleka mtoto shuleni hawezi," alisema Masoud.



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akiwasalimia wananchi wa Songwe katika ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, iliyofanyika hivi karibuni. **PICHA: YASIN IBRAHIM**

# 'Ukatili umehamia kwa watoto wa kiume'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewataka wadau wa haki za binadamu kuelekeza nguvu zao kwenye mapambano dhidi ya ukatili kwa watoto wa kiume kutokana na wanaojihusisha na vitendo hivyo kuhamia kwa kundi hilo kutokana na kampeni nyingi kuwalenga watoto wa kike na wanawake nchini.

Homera aliyasema hayo kupitia hotuba yake iliyosomwa na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Lodrick Mpogoro wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo majaji wanawake wa mikoa ya Mbeya na Songwe.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake nchini (TAWJA) kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake (UN Women).

Homera, alisema kampeni nyingi za kupinga ukatili wa kijinsia zimekuwa zikiwalenga zaidi watoto wa kike na kusababisha ukatili huo kuanza kuhamia kwa watoto wa kiume.

"Nisema tu hapo nyuma tulipokuwa tunazungumzia habari ya ukatili, tulikuwa tukigusa wanawake na watoto, lakini nguvu ilielekezwa kwa watoto wa kike, tunapozungumzia watoto tunazungumza kwa ujumla yaani wa kike na wa kiume kwa hiyo tuwekeze nguvu kote," alisema Homera.

Mwenyekiti wa TAWJA, Jaji Barke Sehel ambaye ni Jaji wa Mahakama ya Rufani, alisema mafunzo hayo yamewashirikisha majaji na mahakimu wanawake wa mahakama zote nchini.

Alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mikakati iliyoanzishwa na chama hicho kuhakikisha wadau wote wa kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wanakuwa na uelewa wa matumizi ya Kitabu cha Mwongozo kwa majaji na mahakimu kuhusu mashauri yanayohusu ukatili wa kijinsia.

Alisema kitabu hicho kiliandaliwa na TAWJA na kuzinduliwa na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye alishauri mafunzo yatolewe kwa wadau wote.

"Tulikuwa na mkakati huo wa kutoa mafunzo kwa wadau likiwamo Jeshi la Polisi, maofisa ustawi wa jamii, mashirika yanayoshughulikia haki za binadamu na madawati ya jinsia, lakini rais alisisitiza jambo hili kwahiyo tumeamua kuanza na kundi hili," alisema Jaji Barke.

Alisema wataendelea kutoa mafunzo hayo kwa majaji na mahakimu katika mikoa mingine nchini kabla ya kuanza kuyatoa kwa wadau wengine.

Makamu Mwenyekiti wa TAWJA, Jaji Victoria Nongwa ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, alisema Tanzania imefanya vizuri kwenye medani za kimataifa katika kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za watoto na wanawake.

Alisema kupitia mkutano wa Mahakama ya Afrika uliofanyika hivi karibuni nchini Algeria, Tanzania ilitajwa kuwa moja ya mataifa yanayofanya vizuri na kwamba mafunzo hayo yataongeza ufanisi zaidi.

# Chunya kunufaika upimaji ardhi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imechaguliwa kuwa miongoni mwa halmashauri saba nchini zitakazonufaika kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Miliki za Ardhi nchini (LTIP) unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mradi huo unatekelezwa nchini kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) na unatajwa kuwa miongoni mwa miradi itakayoleta suluhu ya kudumu ya migogoro ya ardhi nchini.

Mkuu wa Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Furaha Kalinga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ardhi.

Kalinga, alisema lengo la mradi huo ni kuboresha usalama wa miliki za ardhi kwa wananchi waishio mijini na vijijini kwa kuwezesha utoaji hati miliki za ardhi kwenye kila kipande cha ardhi inayopatikana kwenye maeneo husika.

Alisema mradi unalenga kutoa hatimiliki 2,500,000 kwenye maeneo utakakotekelezwa, kwa upande wa wananchi wanaoishi vijijini katika halmashauri za wilaya umelenga kutoa hatimiliki za kimila 500,000.

"Kwa wilaya yetu ya Chunya wastani wa hatimiliki kati ya 75,000 hadi 100,000 zitatolewa kwa wananchi na tunaamini mradi utakuwa na tija kwa wananchi na serikali yetu hasa katika kupangilia matumizi yake," alisema Kalinga.

Alizitaja kazi zitakazofanyika kupitia LTIP kwa halmashauri yake kuwa ni pamoja na kuandaa mpango wa usimamizi wa mazingira na kijamii na kufanya urejeaji na upimaji wa mipaka ya vijiji vyote ambavyo havijapimwa.

Alitaja shughuli nyingine kuwa ni kuviwezesha kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vipatavyo 21 na kufanya utambuzi, upimaji na uandaaji wa hati miliki za kimila kwa wananchi bila malipo.

Mkuu huyo alisema mipango ya matumizi bora ya ardhi imekusudiwa kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

"Tunatarajia baada ya utekelezaji wa mradi huu kupungua kwa mizozo ya mipaka baina ya vijiji ambayo imekuwapo kwa muda mrefu," alisema Kalinga.

Alifafanua mradi huo kutekelezwa kwa zaidi ya miezi miwili kwa wastani wa vijiji vinne kwa muda wa siku 14 mpaka 15.

Alisema Chunya ina vijiji 43, kati ya hivyo 26 vimepimwa na kukabidhiwa vyeti, vijiji 17 havijapimwa, 10 vina mpango wa matumizi bora ya ardhi, 12 viko ndani ya mji na vijiji vitakavyonufaika sasa ni 21.

Halmashauri nyingine zitakazonufaika na awamu hiyo ni Chamwino mkoani Dodoma, Longido (Arusha), Maswa (Simiyu), Mufindi (Iringa), Songwe, Mbinga (Ruvuma) na Tanganyika (Katavi).



## TAMWA yataka uwazi kesi za mauaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimelitaka Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama kushughulikia kwa uwazi kesi za ukatili, udhalilishaji wa kijinsia na mauaji.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana Mkurugenzi wa chama hicho, Dk. Mzuri Issa alipongeza hatua ya mahakama ya kutoa adhabu kali katika kesi ya mwanamke aliyeuawa kikatili na mpenzi wake.

Hivi karibuni Mahakama Kuu Zanzibar ilitoa taarifa kuwa imemuhukumu Haji Jaha Issa (37) kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa makusudi Hajra Abdallah Abdallah (21) kwa kumchoma kisu kifuani, ubavuni na tumboni.

"Taarifa hiyo ilitaja kuwa hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Rabia Hussein Mohammed ambaye aliridhishwa na ushahidi uliotolewa katika mauaji hayo yaliyofanyika Februari 26, 2020 huko Paje, Mkoa wa Kusini Unguja," alisema Dk. Mzuri na kupongea uamuzi huo ambao mahakama umetenda haki.

Alisema TAMWA inaamini kwamba uwazi na utoaji taarifa kwa mahakama ni msingi mzuri wa utawala bora na itaongeza imani kwa wananchi katika kutegemea hukumu za vyombo vya sheria na kupunguza kiwango cha uhalifu kwa vile kitawatisha wanaotaka kutenda makosa hayo. "TAMWA inategemea kuwa Mahakama pamoja na vyombo vingine vya sheria vitaweka wazi taarifa zake kuhusu mashtaka na hukumu ili kufikia matakwa hayo ya nchi na ya kidunia," alisema.

Alisema ni muhimu kwa taasisi hizo kutoa taarifa kila mwezi kuhusiana na mwenendo wa kesi, kueleza mafanikio na changamoto na kuweka mifumo ya kuripoti malalamiko. Kwa mujibu wa kumbukumbu ya TAMWA Zanzibar, wanawake 19 na watoto wanne wameuawa visiwani hapa tangu mwaka 2016 hadi Mei mwaka huu.

Watoto hao Laura Msemwa (23) na Khairat Juma Bakari (28) waliuawa kikatili katika eneo la Bububu Kijichi na Mbuzini Wilaya ya Magharibi A Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Hata hivyo, aliitaka jamii kuendelea kushirikiana na mihimili muhimu ili kuharakisha na kufanikisha uchunguzi wa matukio ya uhalifu na kutenda haki kwa waathirika. Katika hatua nyingine Dk. Mzuri, amesema TAMWA imekemea udhalilishaji wa watoto mitandaoni na kuitaka jamii kuzuia kurekodi watoto watoto kufanyiwa udhalilishaji.

Alisema hatua hiyo imekuja baada ya kusambaa picha na sauti ya mtoto kurekodiwa kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii na watu waliokuwa wakimhoji kinyume na maadili ya uandishi wa habari. "Watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya vitendo vyote vya udhalilishaji, vitisho vya usalama wao na unyanyasaji wa mtandaoni. Sheria inakataza mtu yeyote kutoa taarifa au kuchapisha picha ambayo itapelekea kumtambulisha mtoto aliyeathirika bila ya amri ya Mahakama," alisema.

Dk. Mzuri alitaka serikali kuandaa mkakati imara utakaosaidia kutoa elimu kwa jamii ili kuzuia vitendo vya kurekodi na kusambaza taarifa za udhalilishaji watoto.

# Majaliwa akerwa teknolojia kudhalilisha wanawake, watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kasi ya maendeleo ya teknolojia inaongeza ukatili na udhalilishaji wa kijinsia duniani kutokana na matumizi mabaya.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana katika bustani za Forodhani baada ya kumaliza mbio za hiari za kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Duniani yaliyoandaliwa na Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation kwa lengo la kusaidia wanawake waliopata athari za ukatili wa kijinsia na kutelekezwa na waume zao.

Akizindua mbizo hizo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Majaliwa alisema kuna matumizi mabaya ya mtandao kwa baadhi ya watu wasio na nia njema kwa kuwadhalilisha watu, wanawake na watoto jambo ambalo linapingwa duniani kote.

Alitaka mitandao hiyo kutumika kuelimisha jamii na taifa na wale ambao wanaitumia vibaya kuacha mara moja kufanya hivyo kwa kuwa ni kosa kisheria.

Alisema kila mmoja kwa nafasi yake, anapaswa kuwajibika kupambana na kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa sababu ni mtambuka na bila ya ushiriki wao, vitendo hivyo vitashindwa kutokomezwa katika jamii.

"Kila mmoja kuwa tayari kuwalinda hawa kwa sababu bila ya mama mambo hayaendi na watoto ndio ambao tunaendelea kuwarithisha katika shughuli mbalimbali za maendeleo," alisema.

Majaliwa, alisema vitendo vya ukatili na udhalilishaji vinaendelea kutokea nchini, hivyo ni vyema kufichua matukio hayo yanapotendeka ili kuchukua hatua kwa sababu sheria, kanuni na taratibu zipo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania (SMT) zinahubiri kuwalinda wanawake na watoto na zimeweka sheria kuwalinda, hivyo jitihada hizo zinatokana na sera zilizopo na kila mmoja kushiriki kikamilifu kuhakikisha makundi hayo yanalindwa.

Majaliwa, alisema miongoni mwa jitihada za serikali katika kutokomeza vitendo hivyo ni kuunda madawati ya vituo vya ulinzi na usalama wa mtoto na kutoa huduma za msingi kwa waathirika wa matukio hayo.

Alisema Tanzania Bara kuna madawati 1,850 kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kuripoti matukio ya kudhalilishwa na kunyanyaswa ili hatua zaidi zichukuliwe.

"Madawati haya yanaanzishwa kila ilipo shule ya msingi na sekondari, kwa upande wa sekondari kuna madawati 1,283, na kwa Zanzibar madawati 40 yameundwa katika vituo vya polisi ili kutoa huduma zinazolinda na kuchukua hatua dhidi ya wanaofanya ukatili wa kijinsia," alisema.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema vitendo vya ukatili vimekuwa vikikithiri na wizara yake imekuwa ikipokea changamoto nyingi ikiwamo ya wanawake waliozaa watoto wenye ulemavu kutelekezwa.

Aliipongeza Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation kwa kuandaa mbio hizo kwa lengo la kuwasaidia wanawake waliotelekezwa na waume zao kwa kuzaa watoto wenye ulemavu.

Mkurugenzi wa Asma Mwinyi Foundation, alisema fedha zilizopatikana katika mbio hizo zitawasaidia kuwainua kiuchumi wanawake ambao wamekumbana na kadhia ya kudhalilishwa na waume zao kwa kuzaa watoto wenye ulemavu ili waanzishe miradi ya kujiingizia kipato.

Msaidizi Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Ousmane Niang, alisema zaidi ya wanawake na wasichana milioni 200,045 wanapata changamoto za ukatili na udhalilishaji.

Niang alisema kwa Tanzania kila wanawake na wasichana 25 kutoka umri wa miaka 15 hadi 49 wanadhalilishwa.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akisalimiana na Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alipowasili hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa Ndege, Zanzibar, kuhudhuria ufunguzi wa kongamano la siku mbili la kumuenzi marehemu Maalim Seif, katikati ni mjane Mama Awena Sinani Masoud. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

# TRA yawakumbuka wazee nyumba za serikali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar imeboresha miundombinu ya maji kwenye nyumba za serikali wanamoishi wazee ikiwa ni kuadhimisha wiki ya shukurani kwa walipakodi visiwani hapa.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari katika bonanza la wiki ya walipakodi visiwani hapo, Naibu Kamishna wa Mamlaka hiyo Zanzibar, Saleh Haji, alisema wametumia shilingi milioni 10 kuboresha miundombinu hiyo na kutoa msaada wa vitu mbalimbali kwa wazee hao.

Haji, alisema wiki hiyo kila mwaka hutumika kwa kutoa elimu kwa jamii na zawadi kwa walipakodi ambao ni vinara katika ulipaji kodi.

Alisema kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, serikali ikikusanya kodi ya kichwa ilikuwa ikitegemea mazao yake makuu ikiwamo nazi na karafuu, baada ya matumizi ya fedha hizo kwenda vizuri husafirisha nje ya nchi.

Alisema kutokana na ushindani wa kibiashara duniani, mazao hayo yakapungua uzalishaji na serikali kujiimarisha katika ukusanyaji wa kodi ikiwamo ya manunuzi, uingizaji wa bidhaa na kodi ya mapato.

Alisema maendeleo hayo yamesaidia serikali kujenga miundombinu ikiwamo barabara, hospitali na shule ili kuwanufaisha wananchi.

"Tumeweka siku hii maalumu ili kuwapongeza walipakodi kuona thamani yao na mchango wao mkubwa katika ulipaji wa kodi ambayo huiwezesha serikali kufanya maendeleo kwa wananchi," alisema.

Hata hivyo, alisema katika mwaka wa fedha uliopita, TRA ilikusanya Shilingi trilioni 24 na Zanzibar kupangiwa Shilingi bilioni 455 na kuvuka lengo kwa kukusanya asilimia 100.03.

Mkuu wa Wilaya ya Mjini Magharibi Unguja, Rashid Msaraka, alisema awali suala la ukusanyaji kodi lilikuwa na mivutano baina ya walipakodi na TRA, mabadiliko ya uongozi yamesababisha kuonekana ni jambo la maslahi ya wote.

Maadhimisho hayo yaliambatana na matembezi ya hiari yaliyoanza ofisi ya TRA Kinazini hadi Viwanja vya Mao.

# Wadau waomba sheria mahususi kupinga ukatili wa kijinsia

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa kupinga ukatili wa kijinsia wameiomba serikali kutunga sheria mahususi ya kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia.

Wakizungumza katika uzinduzi wa siku 16 za uanaharakati dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia wadau hao walisema kutungwa kwa sheria hiyo kutasaidia kupunguza vitendo hivyo.

Mwenyekiti wa Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Dk. Monica Mhoja, alisema pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na wadau katika kupambana na vitendo hivyo, lakini bado hakuna sheria mahsusi ya kushughulikia vitendo hivyo.

Pia walipendekeza kuharakisha mchakato wa utungaji wa awamu ya pili ya mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia (MTAKUWA) na kuweka bajeti ya kutosha ya kusaidia kamati zilizoundwa katika utekelezaji wa mpango huo kufanya kazi kwa ufanisi.

Kadhalika, waliomba serikali kufanya mapitio ya kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa na uchakataji wa takwimu za ukatili wa kijinsia ili zioane.

"Kwa hali ilivyo sasa mifumo ya watoa huduma wakiwamo Jeshi la Polisi, Ustawi wa Jamii, Afya, Mahakama na taasisi nyingine, haifanani na hivyo kusababisha mashauri mengi kuendeshwa kwa kukosa ufumbuzi yakinifu," alisema Dk. Mhoja.

"Sote tunafahamu chanzo kikuu cha ukatili wa kijinsia ni mifumo pamoja na mila na desturi kandamizi, hivyo mabadiliko ya kifikra na serikali kwa upande wake ikiwekeza katika sera na sheria, bajeti na mifumo inayozuia na kupambana na ukatili huo utasaidia kutokomeza vitendo hivyo."

Waziri wa Maendeleo, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, alisema serikali inafanya mchakato wa kufanya maboresho kwenye sera na sheria katika eneo hilo zitakazosaidia kuongeza nguvu kwenye mapambano kwenye eneo hilo.

Kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mtoto, Dk. Gwajima alisema, bado wanafanya mchakato kuhakikisha zote zinasomana kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria.

Pia alisema kuna haja kwa jamii kujenga tabia ya kuwaripoti katika vyombo vya sheria wote wanaoshiriki katika vitendo hivyo vya ukatili badala ya kuwaacha mitaani.

"Sasa kuna tabia, yaani watu wanaishia tu kutoa maoni kwenye mitandao pale kunapofanyika vitendo hivyo badala ya kuchukua hatua kwa kuripoti katika vyombo vya dola, vita dhidi ya ukatili ni vya kila mtu," alisema Dk. Gwajima.

Alizitaka halmashauri zote nchini, kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na vitendo hivyo kuanzia kwenye ngazi za mitaa.




Mwanzilishi Mwenza wa Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST), Dk. Gozibert Kamugisha, akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu maandalizi ya shindano la maonesho ya wanasayansi chipukizi, Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Mtendaji wa Karimjee Foundation, Caren Rowland na kushoto ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Dare Impact, Alfred Ngulo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# UTPC yaanzisha kampeni maalum ya elimu siku 16

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UMOJA wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), umeanzisha Kampeni Maalum ya siku 16 ya kutoa elimu kwa jamii ya kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia katika kundi la wanawake na watoto nchini.

Kampeni hiyo maalumu inayoshirikisha zaidi ya waandishi wa habari 1,000 nchini inakusudia kuisaidia serikali katika mapambano ya kuzuia vitendo vya ukatili ambavyo kwa sasa vimekuwa janga kwa taifa.

Akizindua kampeni hiyo mjini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Keneth Simbaya, alisema kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto ni miongoni mwa ukiukwaji uliokithiri wa haki za binadamu.

Kampeni hiyo kwa mwaka huu imebeba kaulimbiu inayoeleza; Wekeza, Zuia Ukatili wa Kijinsia.

Alisema vyombo vya habari vikiandika habari hizo za kutoa elimu kwa jamii kwa ajili ya kuzuia vitendo vya ukatili kwa makundi hayo vitasaidia kuleta mjadala mpana kwenye jamii na jinsi wanavyojadiliana ndio kutaleta mabadiliko.

"Tukilifanya hili jambo kwa dhati litaleta mjadala mpana na hakuna mabadiliko yanayotokea kabla ya watu hawajaelimika na vyombo vya habari haviwafundishi watu kufikiri, lakini linawapa suala la kufikiria," alisema.

"Kikubwa hatupendi kuona hatua zinachukuliwa baada ya tukio kutokea, tunalo jukumu kama waandishi wa habari kutoa elimu ili kuzuia matukio yasitokee, watu wanasema kuzuia ni bora kuliko kuponya," alisema Simbaya.

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa UTPC, Deo Nsokolo, Mjumbe wa Bodi hiyo, Lilian Lucas, alisema wanahabari wana jukumu la kuwa mstari wa mbele la kuwasemea wanawake na watoto ambalo ndio kundi kubwa linaloathirika na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Wapo wanaume wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia, lakini kundi la wanawake na watoto ndio kubwa zaidi linaloathirika na ukatili huo, kama wanahabari wakipaza sauti zao itasaidia kupunguza vitendo hivyo," alisema.

Mwashabani Seif, Mwandishi kutoka Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar, alisema visiwani ni sehemu ya Tanzania watahakikisha wanapaza sauti kwa kushirikiana na UTPC ili kuondokana na janga hilo kwa kuwa waathirika ni watoto na wanawake.

"Watoto ndio taifa la kesho, wasipolindwa na kuwa matunda mazuri itakuwa ni janga kwa taifa kwani humo humo ndio tunategemea kupata viongozi wakiwamo marais, mawaziri na viongozi wengine," alisema Mwashabani.

UTPC itatumia siku hizo 16 katika kutoa elimu ya kuandaa mada na mijadala mbalimbali ikiwamo ndoa na mimba za utotoni, ukeketaji na vitendo vingine ambavyo ni madhara makubwa na wakati mwingine kugharimu maisha ya watu.

# TASAF-III yatekeleza miradi 74 Morogoro

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF-III), Manispaa ya Morogoro, umefanikiwa kutekeleza miradi 74 ikiwamo ya ajira za muda (PWP) yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 600, Manispaa ya Morogoro.

Mratibu wa TASAF Manispaa ya Morogoro, Feliciana Katemana, alisema hayo jana wakati Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Musa Musa, alipotembelea miradi ya TASAF III iliyotekelezwa katika awamu ya kwanza kwenye kipindi cha mwaka 2022/23 ndani ya kata tofauti za manispaa hiyo.

Alisema inatekelezwa kama miradi ya ajira za muda ambayo huwalipa walengwa ujira kutokana na muda wanaofanya kazi usiozidi saa nne kwa siku na hulipwa Sh. 3,000 kwa muda wa miezi sita ya mradi iliyokamilika mwezi Juni 2023.

Pia, wamekamilisha ujenzi wa barabara ya Mfine ya kiwango cha changarawe yenye urefu wa kilometa 0.5 iliyopo Kijiji cha Mfine, Kata ya Luhungo, Manispaa ya Morogoro, iliyogharimu Sh. milioni 2.9 ikiwa ni pamoja na ujira kwa walengwa 26 na vifaa.

Alifafanua kuwa manispaa kupitia TASAF ina miradi 73 ambayo imegharimu Sh. milioni 374 kwa ajili ya kulipa ujira kwa jamii inayozunguka maeneo husika iliyoshiriki kufanya kazi na Sh. milioni 105 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.

Pia alisema wanaendelea na ujenzi mkubwa wa mradi wa ujenzi wa bwalo la chakula kwa wazee wasiojiweza wa Kituo cha Fungafunga kilichopo Manispa ya Morogoro.

Mradi huo unaogharimu Sh. milioni 203, ulianza kujengwa tangu Juni 2023 na unatarajiwa kukamilika Desemba 2023.

Bwalo hilo linasimamiwa na kamati ya ujenzi ya mtaa kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri na litasaidia kuboresha uchumi wa wazee baada ya kukabidhiwa jengo na kufanya shughuli za kuboresha uchumi kwa kuruhusu mikutano mbalimbali kufanyika humo.

Katibu Tawala wa Mkoa, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, kutenga fedha kwa ajili ya kujenga uzio ili kuhifadhi jengo hilo na kuweka vifaa vya kisasa na kuliongezea thamani hasa kwa watu watakaotaka kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo mikutano na sherehe mbalimbali.

Mmoja wa wakazi wa mtaa wa Mfine, Abdalah Kingomela, alishukuru serikali kupitia TASAF kwa kuwajengea barabara ya daraja dogo katika mtaa huo na kusaidia magari kufika kwenye eneo lao yaliyoshindwa kufika tangu nchi imepata uhuru mwaka 1961.

Mwenyekiti wa kituo cha Fungafunga, Joseph Kaniki, alishukuru serikali kwa kuwajali katika mambo mbalimbali kimavazi, malazi na afya huku wakiwajengea kitega uchumi hicho ambacho wanaahidi kukitunza kwa faida yao.

Kaniki alisema kituo hicho kwa sasa kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa majisafi na salama kwa sababu ya kupata maji kidogo yanayotoka mara moja kwa wiki pamoja na ukosefu wa njia ya uhakika ya kufikiwa na wageni mbalimbali kituoni hapo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, alisema bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na daraja katika mto Ngerengere, jirani na kituo hicho umeshapitishwa na wanasubiri Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuanza utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2023/24.

# Kenya yaweka mikakati kukabiliana na mafuriko

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya, William Ruto, amesema serikali yake imeweka mipango ya kuwasaidia raia wake ambao wameathirika na mafuriko yanayotokea kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha kwenye maeneo mbalimbali nchini humo.

Rais Ruto aliyasema hayo jana baada ya kukutana na idara mbalimbali zinazohusika na kukabiliana na majanga Ikulu ya Nairobi ambako alithibitisha kuwa karibia watu 70 wamefariki katika mafuriko hayo huku wengine 36,000

wakipoteza makazi yao baada ya kufurika maji.

Aidha, mkuu wa nchi hiyo alieleza kuwa mvua itaendelea kunyesha, hivyo maandalizi zaidi yanahitajika ili kukabiliana na dharura zinazoweza kutokea.

Hata hivyo kutokana na hali inayoendelea kushuhudiwa kwa sasa nchini humo, Baraza la Mawaziri linatarajiwa kukutana leo, ikielezwa kuwa suala la mafuriko linatarajiwa kujadiliwa kwa mujibu wa wachambuzi wa mambo.

Vile vile kikao hicho kinatarajiwa kujadili mbinu mwafaka zinazohitajika kukabiliana na athari zinazotokana na mafuriko ambayo yameendelea kuwa changamoto kwa raia katika taifa hilo la Kenya.

Nchi iko katika sehemu nzuri ya kukabiliana na athari za mafuriko haswa wakati huu serikali kuu inaposhirikiana na zile za majimbo, alisema Rais Ruto.


Pia Rais Ruto alieleza kuwa wanajeshi watasaidia katika upelekaji wa misaada katika maeneo yaliyoko mbali na ambayo

yamefunikwa na mafuriko ambako pia vitengo vingine vya walinda amani vitatumika kuhakikisha usalama wa raia.

Kando na hayo, Rais Ruto alitoa wito kwa wananchi wake kutumia mvua inayoendelea kunyesha kuboresha na kujiunga katika kilimo.

Mataifa ya Pembe ya Afrika yanakabiliwa na mafuriko yanayosababishwa na mvua kubwa inayoendelea kunyesha, Tanzania ikiwa mojawapo ikifuatiwa na majirani zake Kenya na Somalia.

**RFI**



Mfungwa wa Palestina akikumbatiana na ndugu yake baada ya kuachiliwa kutoka gereza la Israel na kurejea Jerusalem, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Mateka zaidi waachiliwa na Hamas

**GAZA,** PALESTINA

JESHI la Israel limesema Waisrael 13 pamoja na raia wa Thailand wanne wameachiliwa huru huko Gaza kwa

kubadilishana wafungwa wengine 39 wa Kipalestina waliachiliwa na Israel katika Ukingo wa Magharibi.

Ilielezwa kuwa zoezi hilo lilifanyika jana chini ya makubaliano ya pande zote mbili, na kwamba awamu ya kwanza ya

kuwaachilia mateka ilifanyika vizuri Ijumaa, chini ya makubaliano ya muda ya siku nne yaliyosimamiwa na Qatar.

Mrengo wa kijeshi wa Hamas, Al Qassam Brogade, ulisema kuna masuala hayakuwa sawa juu ya uwasilishaji wa misaada kaskazini mwa Gaza na vigezo vya uteuzi wa wafungwa wa Kipalestina wanaobadilishwa na wafungwa wanaoshikiliwa na Hamas, licha ya Israel kukanusha kukiuka masharti ya mkataba huo.

Msemaji wa Hamas, Osama Hamdan alisema jumla ya malori 340 ya misaada yameingia Gaza tangu Ijumaa, lakini ni 65 pekee ndiyo yamefika kaskazini mwa Gaza ambayo ni chini ya nusu ya kile Israel ilikubali. Huku Israel ikielezea kaskazini kama eneo la vita na kwamba Umoja wa Mataifa (UN) una jukumu la kutoa msaada huo.

Ilielezwa kuwa baada ya madai hayo muda mchache baadaye ofisa mkuu wa Palestina aliye karibu na mazungumzo hayo alithibitisha taarifa ya Qatar kwamba mzozo huo umetatuliwa.

Inaelezwa kuwa Hamas ilionyesha kuzishukuru Misri na Qatar kwa kuhakikisha kuendelea kwa mapatano yao ya muda na Israel.

Taarifa zilibainisha kuwa chini ya makubaliano hayo, mateka 50 wa Israel wanawake na watoto wataachiliwa na Hamas kwa muda wa siku nne, wakibadilisha na wafungwa 150 wa Kipalestina.

**WAKUSANYIKA UWANJANI**

Kutokana na utaratibu unaoendelea wa kuwaachilia mateka, jamaa na marafiki wa wale wanaoshikiliwa na Hamas huko Gaza wamekuwa wakikusanyika nje ya Jumba la Makumbusho la Sanaa huko Tel Aviv, katika uwanja ambao sasa unajulikana kama saa kadhaa kabla ya kuachiliwa kwa kundi jingine.

Sigalit Salminis ambaye ni raia wa Israel aliyekuwa akisubiri habari kuhusiana na mpwa wake, Carmel Gat mwenye umri wa miaka 39, ambaye alichukuliwa kutoka Kibbutz, akitumai kwamba anaweza kujumuishwa katika kundi la watu watakaoachiliwa kama sehemu ya mapatano kati ya Israel na Hamas.

Nina matumaini kwa sababu huu ni mwanzo wa mchakato wa watu wetu kurudi nyumbani. Pia tuna wasiwasi kwa sababu watu bado wako mikononi mwa Hamas lakini tunatumai yote yatakwisha, alisema na kuongeza:

Tunataka kila mtu arudi. Sisi wote ni familia moja kubwa sasa.

Ni watu ambao walichukuliwa kutoka kwenye nyumba zao. Hao ni watu wasio na hatia, alisema Salminis.

Pia alieleza kuwa matumaini ya Shirika la Msalaba Mwekundu, ambalo limesaidia katika uhamisho wa mateka, litapewa fursa kwa wale waliosalia kifungoni.

**SHUTUMA KWA ISRAEL**

Wakati hayo yakiendelea mshauri wa vyombo vya habari kwa mkuu wa ofisi ya kisiasa ya Hamas, Taher Al-Nono, alisema kwamba kulikuwa na ukiukaji ndani ya makubaliano ya usuluhishi wa kibinadamu katika Ukanda wa Gaza, ambayo yalianza kutekelezwa Ijumaa asubuhi.

Al-Nono alisema kuwa wanajeshi wa Israel walikiuka makubaliano ya kusitisha mapigano huku wakifyatua risasi dhidi ya Wapalestina wakati wa kipindi cha kusitisha mapigano na

kusababisha kuuawa kwa Wapalestina wawili mjini Gaza.

Alisema kuwa msaada ulioingia katika eneo la kaskazini mwa Gaza ni mdogo sana kuliko ilivyokubaliwa, akieleza kuwa

Hamas inafuatilia utekelezaji wa kila kifungu cha makubaliano kwa undani, lakini Israel inatishia utekelezaji wa makubaliano hayo kikamilifu.

**MTAZAMO WA WAPALESTINA**

Wapalestina wengi wanasema Israel inaharamisha vitendo vya upinzani vinavyofanywa na watu ambao ardhi yao inakaliwa kimabavu huko Ukingo wa Magharibi.

Kwa mujibu wa Rais wa Jumuiya ya Wafungwa wa Palestina, Abdallah Zughary, robo ya wakazi katika ukingo huo wamezuiliwa kwa muda katika jela ya Israel kama adhabu ya pamoja.

Na kwamba zaidi ya watu 3,000 wamekamatwa tangu mashambulizi hayo kuanza, ikiwa ni pamoja na karibu watoto 900.

Wengi wa wafungwa hawa wamezuiliwa bila kufunguliwa mashtaka na wengi wao ni raia, wasiofungamana na aina yoyote

ya chama cha kisiasa au kikundi cha wapiganaji. Tangu Oktoba 7, wafungwa hao hawajakutana na familia wala wanasheria wao.

Na sita kati yao wamekufa, alisema.

Pia iliishutumu Israel kwa kutumia mfumo wa haki kama sera ya kulipiza kisasi. **BBC**

# MBEYA KWANZA YAREJEA TENA KILELENI LIGI YA CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza juzi, ilirejea kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship kwa kishindo baada ya kuibamiza Cosmopolitan mabao 3-2 katika mechi ya raundi ya 12 ya ligi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona, kusaka timu mbili zitakazopanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, huku moja ikisubiri mechi za mchujo.

**Mbeya Kwanza imeiengua kileleni TMA iliyokuwa inaongoza kwa wiki nzima, ikishushwa hadi nafasi ya pili baada ya kulazimishwa suluhu dhidi ya Mbeya City.**

Mabao ya washindi yalifungwa na Ramadhani Kapera, akipachika mawili dakika ya 14 na 55 na Jocob Benedicto dakika ya 35, huku ya Cosmopolitan yakiwekwa wavuni na Mfaume Said dakika ya 27 na Benjamin Mwakifunga dakika ya 73.

Kwa ushindi huo, Mbeya Kwanza inafikisha pointi 26 na mabao 19, ikikaa kileleni mwa msimamo wiki hii, huku TMA ikishuka nafasi ya pili ikiwa na pointi 26 pia, lakini ina mabao 11 tu ya kufunga.

Mabao mawili aliyofunga Ramadhani Kapera yanamfanya kukaa juu ya orodha ya wafungaji bora akifikisha jumla ya mabao tisa mpaka sasa.

Salim Aiyee wa Mbuni FC na Edgar William wa KenGold wanashika nafasi ya pili wakiwa na mabao manane kila mmoja, Abdulkarim Segeja wa Copco ana mabao saba, huku Boban Berege wa Biashara United, Kassim Shaibu wa Green Warriors na Maulid Shaaban wa Mbeya City wakiwa na mabao matano kila mmoja.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akitoa cheti maalumu kwa Meneja wa Rasilimali Watu wa TPA, Musa Saidi Msabimana, baada ya TPA kutangazwa washindi wa jumla wa michezo ya SHIMMUTA 2023, iliyomalizika jana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

# *TPA mabingwa wa jumla mashindano SHIMMUTA 2023*

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imetangazwa kuwa mshindi wa jumla katika michuano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) 2023, iliyomalizika jana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Meneja Rasilimali Watu wa TPA, Mussa Msabimana, akizungumza na waandishi wa habari baada ya TPA kutangazwa mshindi wa jumla, alisema mafanikio hayo yametokana na maandalizi mazuri yaliyofanywa na timu zao kwa ajili ya michuano hiyo.

Katika mashindano hayo, TPA imetwaa ubingwa kwa timu zake za mpira wa kikapu (basketball) ambayo iliinyuka TRA kwa jumla ya vikapu 66-25 katika mchezo wa fainali.

Alisema kwa upande wa mpira wa pete (netball), TPA imeigaragaza timu ya TANESCO kwa vikapu 53-36 huku katika mchezo wa kamba upande wa wanawake ikiishinda timu ya TPDC.

Alisema katika mchezo wa kamba timu ya wanaume TPA imeichapa TBS na kunyakua ubingwa na mchezo wa drafti kwa wanawake, Celina Simon, akiibuka mshindi wa tatu.

"Kwenye kukimbia ndani ya magunia TPA imetwaa ubingwa wa kwanza. Kwa upande wa mchezo wa riadha mita 100 wanaume, TPA imeibuka mshindi wa pili na kupata medali ya fedha huku mita 200 wanaume ikitwaa ushindi wa kwanza," alisema.

Pia, alisema katika mchezo wa riadha mita 400 wanawake, imetwaa ushindi kwa kushika nafasi ya pili na mita 400 uliohusisha wanaume wakiwa nafasi ya kwanza.

Alisema kwa upande wa mita 800 wanawake, wametwaa nafasi ya pili huku mita 1,500 wanawake wakitwaaa ushindi wa tatu.

"Mita 1,500 wanaume wameshika nafasi ya pili na mita 5000 wanaume wamepata nafasi ya tatu.

"Katika ushindi wa jumla upande wa riadha wanawake imeshika nafasi ya tatu huku mshindi wa jumla wanaume akishika nafasi ya kwanza na upande wa wazee riadha imeibuka mshindi wa jumla," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliipongeza TPA kwa kuibuka mshindi wa jumla katika mashindano hayo.

"Ninaipongeza TPA kwa mafanikio haya na ninazihamasisha taasisi nyingine kujipanga kwa ajili ya michezo ya mwakani," alisema.

# TRA bingwa wa soka michuano SHIMMUTA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TIMU ya Soka ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imetawazwa mabingwa wa michuano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA), baada ya kuitupa nje TANAPA kwa mikwaju ya penati 4-2, katika mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Jamhuri jiijini Dodoma jana.

Timu hizo hadi dakika 90 za mchezo zinamalizika, zilitoka sare tasa katika michuano hiyo iliyofikia ukingoni jana.

Mabingwa hao kwa mara ya pili mfululizo walizawadiwa kombe pamoja na medali zilizotolewa na waandaaji wa mashindano hayo.

Akizungumza baada ya ushindi huo, Nahodha wa TRA, Emmanuel Boniface, alisema siri kubwa ya ushindi huo ni pamoja na mazoezi ambayo wamekuwa wakifanya kila siku kabla ya mashindano hayo kuanza.

Alisema wanaushukuru uongozi wa TRA ambao umekuwa ukiwapa ushirikiano kabla na wakati wa michuano hiyo iliyokuwa na ushindani mkubwa TANAPA ikiibuka mshindi wa pili.

Naye Mkurugenzi wa Elimu ya Walipakodi TRA, Richard Kayombo, alisema wamefurahishwa na ushindi huo ambao wanaupata kwa mara ya pili mfululizo, hivyo wataenda kuendelea na mazoezi ili mwakani waweze kuibuka washindi kwa mara nyingine.

# Twiga Stars yapania kuiua Togo WAFCON

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Wanawake Tanzania (Twiga Stars), Diana Mnali amesema kutokana na mazoezi wanayoyafanya hawategemei kupoteza katika mchezo wa mwisho wa kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON) dhidi ya Togo.

Twiga Stars inaendelea na maandalizi ya kujiandaa na michuano hiyo ya WAFCON, dhidi ya Togo mchezo utakaochezwa Alhamisi wiki hii katika Uwanja wa Azam, Chamazi Dar es Salaam saa 10:00 alasiri na marudiano Desemba 5, mwaka huu nchini Togo.

Akizungumza na Nipashe jana, Diana alisema wanaendelea vizuri na maandalizi yao kuelekea mchezo wao wa mwisho wa kusaka tiketi ya kufuzu fainali hizo kwa kuanza na ushindi nyumbani.

Alisema mbali na kufuata maelekezo ya benchi lao la ufundi, lakini wanapokuwa kambini wanahimizana juu ya kufanya vizuri katika mchezo ambao ni muhimu kushinda kwa sababu ya kutafuta nafasi ya kwenda kucheza fainali.

## ZISIKUPITE

**RAMSDALE KWA MKOPO**
KLABU ya Wolverhampton Wanderers inamtaka mlinda mlango wa Arsenal, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 27, kwa mkopo Januari na matumaini ya kumnunua msimu wa majira ya joto. (***Star***)

**COOPER KUTI KAVU FOREST**
KOCHA wa Nottingham Forest, Steve Cooper yuko chini ya shinikizo, huku mmiliki wake, Evangelos Marinakis akizidi kufadhaishwa na matokeo ya hivi karibuni. (***Mail)***

**SPURS YAMTAKA MARATO**
KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na beki wa Benfica, Morato, lakini klabu hiyo ya Ureno inasita kumuuza Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 22 Januari. ***(Record via Sport Witness)***

**TONALI KUZUIA USAJILI**
UWEZO wa Newcastle United wa ununuzi katika dirisha la usajili la Januari utaathiriwa na iwapo mshahara wa kiungo wa kati wa Italia, Sandro Tonali unaweza kupunguzwa huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, akitumikia adhabu ya kufungiwa miezi 10 kwa kukiuka sheria za kamari. ***(Telegraph***)

**ARSENAL NA NEVES**
ARSENAL haina nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Al-Hilal na Ureno, Ruben Neves, huku Mbrazil Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, akiwa mlengwa wao mkuu katika safu ya kati Januari. ***(Fabrizio Romano***)

**LLORIS KUSITISHIWA MKATABA**
KLABU ya Tottenham Hotspur iko tayari kusitisha muda uliosalia wa mkataba wa Hugo Lloris baada ya mlinda lango huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 36, kutofautiana na kocha Ange Postecoglou... (***Football Insider***)

**ECHEVERRI AFUATILIWA MADRID**
REAL Madrid, Paris St-Germain na Manchester City zinamfuatilia mshambuliaji wa River Plate na Argentina mwenye umri wa miaka 17, Claudio Echeverri, 17. (***Sport)***

**CAMARDA AWANIWA LIVER**
CHELSEA, Liverpool na Manchester City zina nia ya kumsajili mshambuliaji chipukizi wa Italia, Francesco Camarda, ambaye alicheza mechi yake ya kwanza ya AC Milan Jumamosi akiwa na umri wa miaka 15. (***90Min)***

**MARTIAL AIVUTIA FENERBAHCE**
KLABU ya Fenerbahce inavutiwa na mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 27, na watajadili mkataba na Manchester United wakati 'Mashetani Wekundu' hao watakaposafiri hadi Istanbul kucheza na Galatasaray kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Fotomac)***

**MADRID YAMKATAA ICARDI**
REAL Madrid wamekataa kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 30, kutoka Galatasaray Januari. ***(Athletic***)

**CHALOBAH BASI TENA**
KLABU ya Bayern Munich na Tottenham Hotspur zimepunguza nia yao ya kutaka kumsajili, mlinzi wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24, Trevoh Chalobah, ambaye yuko huru kuondoka Stamford Bridge Januari. (***Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# CHELSEA SASA YAMTIBUA POCHETTINO AKILIA KIPIGO

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, amesema kipigo cha mabao 4-1, kutoka kwa Newcastle United Jumamosi kinamfanya kuwa "na hasira sana" na kinakatisha tamaa huku akikitaja kiwango cha timu yake hiyo kuwa kibaya zaidi kwa msimu.

**Huu ulikuwa mchezo mbaya zaidi wa msimu wetu hadi sasa, tunahitaji kujifunza katika...**

Chelsea iliingia kwenye mchezo huo baada ya matokeo chanya dhidi ya Tottenham Hotspur na Manchester City, lakini wakasambaratika kipindi cha pili mbele ya Newcastle wakifunga mabao mawili ndani ya dakika moja pamoja na kadi nyekundu kwa nahodha wao, Reece James.

"Huu ulikuwa mchezo mbaya zaidi wa msimu wetu hadi sasa," alisema Pochettino baada ya kutazama mchezo huo akiwa jukwaani kutokana na kufungiwa.

Aliongeza: "Tulikuwa katika kila changamoto, hatukushindana. Hatukuonesha tunachezea kitu muhimu. Hilo ndilo linalonifanya nikasirike na kunikatisha tamaa.

**"Tunahitaji kujifunza katika michezo hii, ni nini kinani fanya niwe na furaha sana, nina hasira sana kwa sababu tunapaswa kuonesha utu na tabia zaidi."**

Pochettino alisema kukosekana kwake hakukuwa na athari huku timu yake ikijitahidi kushindana dhidi ya Newcastle, lakini ni wazi alichanganyikiwa na kiwango cha Chelsea.

"Hatuwezi kukosa fursa ya aina hii ya kuonesha ubora wetu. Tulitoka Tottenham na Man City, na kote duniani watu waliisifu Chelsea," alisema Pochettino.

"Huu ulikuwa mchezo wetu mbaya zaidi msimu huu. Ilikuwa ngumu kuwa kwenye viti. Hatuwezi kulalamika kuhusu matokeo, hatukusoma mchezo tangu mwanzo," aliongeza.

Kocha Eddie Howe aliwataja makipa watatu kwenye benchi la Newcastle, huku tatizo la majeruhi la klabu hiyo likifanya wachezaji 13 kukosekana.

"Ulikuwa ushindi muhimu kwetu katika hali tuliyonayo na rasilimali nyingi... ukiangalia wachezaji tunakosa ilikuwa ni kiwango kikubwa," alisema alisema.



# KLOPP AFURAHIA SARE NA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

JURGEN Klopp amesema Liverpool "walifaulu mtihani" katika sare ya bao 1-1 na Manchester City kwenye Uwanja wa Etihad juzi, Jumamosi.

Trent Alexander-Arnold alifunga bao la kusawazisha kipindi cha pili na kufutilia mbali furaha ya bao la 50 la Erling Haaland kwenye Ligi Kuu ya England.

Klopp alikiri kuwa alifurahishwa na pointi kuliko Pep Guardiola na akasema timu yake imethibitisha tabia yao katika majaribio ya mapema ya ubingwa.

"Kwetu, nadhani ilifaulu mtihani, sina uhakika kama ulikuwa mtihani," alisema Klopp.

"Katika biashara ambayo hakuna mtu ana wakati, ni ngumu sana kuiuliza na kuitumia.

"Mwaka jana tulikuwa na timu ambayo ilicheza kwa muda mrefu pamoja na tukawa chini ya gurudumu hapa (katika kipigo cha mabao 4-1) na hatukuwa na nafasi.

"Leo (juzi) tulikuwa na nafasi. Ukiuliza nani alikuwa na uwezekano mkubwa wa kushinda mchezo huo ni City, hiyo ni wazi. Tunataka kuwa tayari kuwapa mchezo unaofaa na ndivyo tulivyofanya."

City, wakati huo huo, waliachwa na uamuzi wa mwamuzi Chris Kavanagh kukataa bao la Ruben Dias na matokeo kuwa 1-0.

Dias alifunga akiwa nje ya uwanja baada ya Alisson kupangua krosi, lakini Manuel Akanji, akahukumiwa kuwa alimchezea vibaya kipa wa Liverpool.

Baadaye, Guardiola alisema hajaona jibu la tukio hilo, lakini alirejea bao la ushindi la Newcastle United dhidi ya Arsenal mapema mwezi huu, ambalo lilifungwa na Anthony Gordon licha ya Arsenal kupinga kwamba Joelinton alimsukuma Gabriel nyuma.

"Sikuitazama, lakini nilikuwa na mahojiano matano na yote yaliniuliza swali moja kwa hiyo labda uliitazama vizuri kuliko mimi," Guardiola alisema.

# Xavi: Barca lazima ibadili mtazamo kushinda mataji

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez alisema Barcelona lazima wabadili mawazo yao ikiwa wanataka kuwa na mafanikio msimu huu baada ya kutoka sare ya bao 1-1 na Rayo Vallecano kwenye LaLiga Jumamosi.

Bao la kujifunga la Florian Lejeune kipindi cha pili lilifanya matokeo kuwa 1-1 baada ya lile la kwanza la Unai Lopez kuwafanya Rayo kuwa mbele.

Barca, ambao walianza wikendi katika nafasi ya tatu kwenye LaLiga, pointi nne nyuma ya viongozi Girona, sasa wameshinda mechi mbili pekee kati ya tano zilizopita katika michuano yote.

"Nadhani ulikuwa ni mchezo wa nusu mbili," kocha wa Barca Xavi alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Katika kipindi cha kwanza, tulitawala, lakini hatukuenda kwa mchezo, hatukuwa wakali.

"Tulikosa mawazo kama hayo. Ikiwa tunataka kushinda mataji msimu huu, lazima tubadilishe mawazo yetu.

"Kipindi cha pili kilikuwa kizuri, lakini hakikutosha. Tuliamka kwa kuchelewa. Tulifanya tulichotaka: kutawala na kutengeneza nafasi. Tungeweza kufunga zaidi.

"Lakini lazima tushinde michezo hii ikiwa tunataka kushinda LaLiga, kwa hivyo tunapaswa kujikosoa pia, na kuimarika. Lazima tuwe karibu na utendaji wa kipindi cha pili."

Matokeo hayo yataongeza shinikizo zaidi kwa Xavi kabla ya mechi muhimu nyumbani dhidi ya Porto, Atletico Madrid na Girona katika wiki mbili zijazo.

"Ni kawaida kwamba kuna ukosoaji, lakini najua tunaweza kubadilisha hili, kuna muda mwingi," alisema.

"Baada ya kushinda LaLiga na Super Cup msimu uliopita, labda mawazo yetu yameshuka kidogo. Huwezi kuruhusu hilo, wala kutoka kwangu kama kocha au wachezaji. Tunapaswa kutoa zaidi."





# Arteta asifu ujasiri wa Ramsdale

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema mlinda mlango, Aaron Ramsdale, alionesha ujasiri baada ya kuepuka makosa mawili ya kipindi cha kwanza katika ushindi wa bao 1-0 wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Brentford, Jumamosi.

Kai Havertz aliibuka kidedea kwa bao la ushindi kwa kichwa na kuipeleka Arsenal kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, lakini Ramsdale, kutokana na kuanza kwake ligi kwa mara ya kwanza tangu Septemba, alikuwa gumzo kwenye mechi hiyo.

Kushushwa kwa Ramsdale kwenye benchi nyuma ya David Raya kumezua mshangao, hata hivyo, alipewa nafasi yake ya kung'ara, lakini nusuru aisababishie matatizo Arsenal kwa makosa yake mawili.

Shuti la Bryan Mbeumo lilimshinda na Declan Rice alikuwa karibu na kuokoa hatari, halafu akaupangua mpira kwenye eneo lake la hatari na kuuweza kuidhibiti.

"Ujasiri. Ana ujasiri mkubwa na haiba kubwa na hilo ndilo tunalohitaji," alisema Arteta alipozungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Hii ni soka. Nina furaha sana na timu. Jinsi timu ilivyocheza kwa bao safi. Tunaendelea."

Arsenal hawakuwa katika ubora wao na sare ingekuwa matokeo ya haki, lakini Havertz aliyetokea benchi, aliamsha shangwe kubwa kwa kufunga bao lake la pili msimu huu.

"Huo ndio uzuri wake. Mambo yakija rahisi, huyathamini. Yeye ni mfano kwetu sote kufanya kile unachopaswa kufanya unapokuwa na matatizo," alisema Arteta kuhusu fowadi huyo wa Ujerumani.

Arsenal wana pointi 30 mbele ya Manchester City wenye pointi 29, huku Liverpool wakiwa na pointi 28, ingawa bado kuna safari ndefu, Arteta alisema kushika nafasi ya kwanza ni hisia nzuri, hasa katika mechi yake ya 200 akiinoa klabu hiyo.

"Ninapenda kushinda na tuko juu kwenye jedwali na hapa ndipo tunapopaswa kutaka kuwa. Kwangu pia ilikuwa siku maalum - michezo 200 na ninataka kusema asante sana kwa kila mtu anayefanya kazi yangu inafurahisha sana," alisema Mhispania huyo.

## HABARI MICHEZO

# HARMONIZE AIPUA ALBAMU YAKE YA NNE 'VISIT BONGO'

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Tanzania anayetamba kwa kasi katika chati ya muziki, Rajabu Abdul maarufu Harmonize, kwa mara nyingine tena amewatikisa mashabiki kote duniani kwa kutoa albamu yake ya nne iliyokuwa ikisubiriwa sana ya 'Visit Bongo'.

Albamu hiyo yenye nyimbo 14 ambayo inadhihirisha umahiri wake katika miondoko ya Bongo Flava, Afrobeat, Rnb na Amapiano, inawaalika mashabiki kutembelea mandhari mbalimbali za kuvutia za Tanzania.

Albamu hiyo imesheheni nyimbo za: Personal Trainer, Hallelujah, Best Woman, Side Nigga, Sijalewa, Boss, Wangu Mimi, Zanzibar (ikimhusisha Bruce Melodie), Sijui, Tena, Hawaniwezi, Dear X, Single Again Remix (ikimhusisha Nkosazana Daughter) na Single Again.



Jina la albamu hiyo, Visit Bongo, linatumika kama wito kwa mashabiki wa Harmonize popote walipo duniani kutembelea utajiri wa wanyamapori na utamaduni wa Tanzania.

Wimbo wa 'Best Woman' unaelezea nafasi ya kipekee moyoni mwa Harmonize kuhusiana na mama yake kipenzi, Mama Konde (Mama Harmonize), na kinamama warembo wote duniani. Ni heshima ya dhati, upendo na uthabiti unao- jumuishwa na kinamama ulimwenguni.

Visit Bongo ina ushirikiano unaovuka mipaka, ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa Bruce Melodie wa Rwanda kwenye wimbo 'Zanzibar' na remix ya kuvutia kwenye wimbo wa 'Single Again' inayomhusisha Nkosazana Daughter wa Afrika Kusini.

Albamu hiyo ni toleo la nne la Harmonize, kutokana na mafanikio ya 'Afro East', 'Shule ya Upili' na 'Made for Us'.

Katika albamu ya Visit Bongo, Harmonize analenga kutoa kanda ya muziki ambayo itawavutia mashabiki wake wa nyumbani, ikitoa mchanganyiko wa aina ya muziki ambao wanaupenda.

Matarajio tayari yanaongezeka kwa mradi ujao wa Harmonize, ambao unaahidi safu tofauti zaidi na mwelekeo kuelekea soko kubwa la kimataifa.

Akizungumzia albamu hiyo, Harmonize alisema: "Kwa albamu ya 'Visit Bongo', nilitaka kutengeneza albamu ambayo inawakilisha moyo na nafsi ya Tanzania. Kila wimbo ni kusherehekea utamaduni wetu, sauti zetu, kuwakaribisha mashabiki duniani kote kufurahia uzuri wa 'Bongo.' Hii ni albamu maalum kwa ajili yangu, na natumaini itamvutia kila mtu atakayeisikiliza."



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akimpongeza Ofisa Rasilimali Watu Mwandamizi wa Kituo cha Mikutano cha Aicc Arusha, Eliasenya Nnko, baada ya kutwaa ubingwa wa vishale (Darts) kwenye michuano ya SHIMMUTA 2023, iliyomalizika jana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *AICC mbabe tena Vishale SHIMMUTA*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya AICC iliyoshiriki kwenye mashindano ya Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi nchini(SHIMMUTA), imeendeleza ubabe kwenye mchezo wa vishale (darts) kwa kuchukua ushindi kwa wanawake kupitia kwa mchezaji wake, Eliasenya Nnko.

Michezo hiyo iliyohitimishwa jana kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ambaye alimwakilisha Dk. Damas Ndumbaro, alitoa zawadi kwa Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi yaliyoshinda kwenye michezo mbalimbali.

Mbali na kushiriki mchezo wa vishale, timu ya AICC ilishiriki michezo ya pool table, riadha, bao, karata na mbio za magunia na kufikia hatua mbalimbali ikiwamo nusu fainali.

Mashindano hayo ya SHIMMUTA yenye kauli mbiu 'Michezo ni Afya na Uchumi, Tuwekeze kwenye Miundombinu ya Michezo kwa Afya Bora na Uchumi Himilivu! Kazi Iendelee', yalianza Novemba 12, kwa kufunguliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko Novemba 17, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

# Wachezaji Simba SC wawekwa kitimoto

INATOKA UK 24

moja kwa moja Botswana kuunga na timu hiyo.

Katika hatua nyingine, Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena, amesema hajafurahishwa na sare ya bao 1-1 waliyoipata dhidi ya Asec Mimosas kwenye uwanja wa nyumbani malengo yao yalikuwa ni kukusanya pointi tatu Benjamin Mkapa.

Alisema walianza vema mchezo na kupata bao la uongozi, kipindi cha pili hawakucheza vizuri wakaruhusu bao, lakini wameyapokea matokeo hayo kwani ndivyo mpira ulivyo.

"Binafsi tulipofungwa bao la kusawazisha nilipatwa na hasira maana tuliiandaa timu vizuri na kupunguza makosa, lakini kosa moja bao moja ndio mpira, sijafurahishwa na kitu hicho.

"Kocha mkuu anapaswa kuja mapema maana ni kocha mkubwa naamini atakuja kutupatia kila kitu tunachokihitaji ili kututoa kwenye hali tuliyo nayo na mimi niko hapa kumpa sapoti na kumsaidia ili tuweze kutimiza malengo yetu," alisema Cadena.

Alisema wanasahau matokeo yaliyopita sasa wanaangalia mchezo ujao wanaoenda kucheza ugenini, lakini ujio wa kocha mkuu anaamini kila kitu kinakwenda kubadilika.

Kocha wa Asec Mimosas, Julien Chevalier, alisema ulikuwa mchezo muhimu kwao kupata matokeo mazuri na amefurahishwa na kiwango kilichooneshwa na wachezaji wake licha ya kutokuwa na uzoefu na michuano mikubwa.

"Tumecheza mchezo mzuri kwa kiwango kizuri, ninajisikia fahari kwa kikosi changu kipindi cha kwanza hatukuwa na wakati mzuri, lakini nafikiri tulipaswa kushinda kipindi cha pili si matokeo mabaya kwetu.

"Tulikuwa na mchezo mzuri, bado kikosi changu kina baadhi ya wachezaji ambao hawana uzoefu na mashindano makubwa, lakini wameonesha uwezo mzuri naamini kadiri muda unavyozidi kwenda kwenye mashindano haya wachezaji wangu watapata uzoefu zaidi kwa sababu ni hali ya mchezo ulivyo," alisema Chevalier.

# Michezo

Jumatatu Novemba 27, 2023

Nipashe




Chelsea sasa yamtibua Pochettino UK. 21



Mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibanzonkiza (chini), katika harakati za kuipigania timu yake dhidi ya mchezaji wa Asec Mimosas kwenye mechi ya Kundi B ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# YANGA YAIONYA AL AHLY KWA MKAPA JUMAMOSI

## ●●● Yasema inakuja wakati mbaya, huku ikiweka wazi robo fainali ni lazima, hivyo...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema inataka kuwafuta machozi ya kufungwa mabao 3-0 dhidi ya CR Belouizdad, kwa kushinda mechi yao Jumamosi dhidi ya Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri, itakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza alfajiri ya kuamkia jana baada ya kurejea kutoka nchini Algeria, ilipokwenda kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya timu hiyo, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema Al Ahly wamekuja wakati mbaya, ambao Yanga wanahitaji furaha kwa udi na uvumba baada ya kupoteza mechi ya kwanza.

"Sisi msimu huu tunaitaka robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tumeanza kwa kupoteza mchezo wa kwanza dhidi ya CR Belouizdad na hii inakumbusha msimu uliopita, tulianza vibaya kama hivi kwenye Kombe la Shirikisho, tulivyorudi nyumbani, moto halisi wa Yanga ulianza kuonekana kwa hiyo naamini Jumamosi ijayo moto utawaka haijalijalishi anakuja nani.

"Tunajua Al Ahly ni timu kubwa, lakini kuelekea kwenye mechi hii imekuja wakati mbaya ambao Yanga tunahitaji furaha, tumeshatoka kupoteza mechi yetu, hakuna kiswahili Yanga tunataka kufurahi Jumamosi," alisema Kamwe.

**Alisema kikosi cha Yanga haki takuwa na mapumziko yoyote, badala yake kitakwenda moja kwa moja kambini kwa ajili ya mechi hiyo.**

"Hakuna muda wa kupumzika kwa sababu wanachama na mashabiki wa Yanga wanachokitaka ni pointi tatu za nyumbani, wanataka furaha, benchi la ufundi na wachezaji wanajua hilo kwa hiyo wameanza kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwa ajili ya mechi hiyo, tunataka pointi tatu za nyumbani," alisema.

Akizungumzia hali ya kipa wao namba moja raia wa Mali, Djigui Diarra, ambaye hakukaa langoni kutokana na maumivu ya bega, alisema anaendelea vizuri, lakini kukaa au kutokaa langoni katika mechi ya Jumamosi kutategemea ripoti ya madaktari.

"Alikuwa na tatizo la bega na ndiyo maana alikosa mechi dhidi ya Coastal Union, hata alipoenda kwenye majukumu yake ya timu ya taifa hakucheza vile vile, madaktari wamemshauri ni bora akakaa nje kidogo ili apone kwa asilimia 100 kuliko akajilazimisha halafu shida ikawa kubwa zaidi.

"Tupo kwenye Ligi ya Mabingwa kila taarifa huwa ni muhimu, ukiitoa unampa ahueni mpinzani, anajiandaa kutokana na mapungufu ulionayo, benchi la ufundi lilishauri taarifa kama hizi tuzihifadhi ili kutotoa fursa kwa mpinzani kujua taarifa za kiufundi kuelekea kwenye mchezo huu," Kamwe alifafanua.

# Wachezaji Simba SC wawekwa kitimoto

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia kutojituma ipasavyo katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast juzi, Jumamosi, uongozi wa klabu hiyo umetangaza 'hali ya hatari' kwa wachezaji wao, imeelezwa.

Simba ililazimishwa sare ya bao 1-1 katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku wachezaji karibu wote wakionekana kutokuwa fiti vya kutosha kuhimili mikikimikiki ya wapinzani wao hao, ambao walikuwa wakikimbia vema kwa dakika zote 90.

Baada ya mchezo huo, uongozi ulikutana na wachezaji na kuwaeleza kutoridhishwa na kiwango na morali ya timu katika mechi hiyo.

Nipashe ambalo lilikuwapo uwanjani hapo kwa muda wote huo, lilifanikiwa kuongea na kiongozi mmoja, ambaye alisema Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alitaka kujua tatizo kutokana na kutocheza kwa kiwango kizuri.

"Viongozi kwa pamoja wametoa angalizo kwa wachezaji na kuwaambia kama mtu anajiona hawezi kuitumikia timu hiyo basi aweke wazi ili kupewa chake na kusepa," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza kuwa baada ya mchezo huo wachezaji hawakuruhusiwa kwenda nyumbani na wote kutakiwa kuingia kambini na Alhamisi kuondoka kuelekea nchini Botswana katika mchezo wa pili wa Kundi B dhidi ya Jwaneng Galaxy.

Kuhusu kocha mpya, Abdelhak Benchikha, alisema kuna mambo mawili kuwa anaweza kutua nchini leo au kwenda

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >